

Wametishwa

● Askofu Bagonza, Dkt Nshala, Mwabukusi roho juu

VITISHO dhidi ya raia wa Tanzania wenye mawazo mbadala kushauri serikali vinazidi kushamiri.

Habari Uk. 6&7

Askofu Bagonza

Dkt. Nshala

Mwabukusi

Makamanda wa Polisi nchi nzi-
ma walikuwa wanatoa taarifa za
uhalifu wa 'wasiojulikana,' serika-
li inalalamika, wanaharakati wa-
nalalamika. Kesi nyingine mpaka
zimesahaulika..." Askofu Bagonza

ACT-Wazalendo yaibua mazito deni la taifa Uk. 14

Kwa heri Msuya...



Rais Samia Suluhu Hassan, akitoa heshima za mwisho kwenye jenze lenye mwili wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu mstaafu Cleopa Msuya katika viwanja vya Karimjee Jijini, Dar es Salaam, jana. (Picha na Ikulu)

Pambazuko
lafanikisha
fedha
kurejeshwa

GAZETI la Pambazuko limefanya kazi yake. Limewezesha wananchi tisa kurejeshwa fedha zao baada ya kutapeliwa. Hatua hiyo imefanikiwa baada ya habari iliyoandikwa na gazeti hili, kufika kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kagera... Uk. 8



Tazara na
hadithi
ya kapu
lililotoboka

Habari Uk. 20

Tahariri/Katuni

Hili la kutishia uhai lisizoeleke

TANZANIA imekuwa nchi yenye taarifa za kuogofya. Nyingi zikibeba ujumbe wenye vitisho vya kutesa, na hata kutishia kakatisha haki ya kuishi kwa baadhi ya wananchi.

Wenye kupokea vitisho hivyo - wengi ni wale wanaozungumza kupitia vyombo mbalimbali wakionya au kutoa ushauri kuhusu baadhi ya mienendo au uamuzi wa viongozi, taasisi na hata vyombo vya ulinzi na usalama.

Wanaofanya hivyo, ni haki yao kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaruhusu kuwepo kwa uhuru mpana kwa kila mwananchi kutoa maoni yake kuhusu mienendo ya serikali yake.

Kamwe siyo kosa kukosoa na kwenda kinyume na misimamo ya serikali au hata viongozi kuhusu hatua au jambo fulani linalohusu nchi yetu.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, isivyokuwa bahati, kumeibuka tabia ya hovyoyawatafuta wanaoonekana kupinga baadhi ya misimamo na uamuzi wa serikali na kuwatisha kuwa “watakiona cha mtema kuni,” endapo wataendelea kukosoa serikali yao.

Kibaya zaidi wanaotishia kuwafanyia unyama watu wakosoaji, ni “watu wasiojulikana” ambao sasa wanaonekana kuwa na nguvu

kubwa kutokana na kwamba “hawakamati-ki” na yeyote wala chombo chochote.

Kutokamatika kwao kunawafanya kujenga kiburi na mazoea ya kutisha, na pengine wameweza kufanya unyama wao dhidi ya watu hao kwa kuwateka, kuwapoteza na hata kuua.

Sisi Pambazuko tunalaani hatua ya watu hao wasiojulikana, kwani wanaharibu taswira ya Mama Tanzania na watu wake.

Kuteka, kutesa, kupoteza na hata kuua, ni mambo yanayovuruga zaidi sifa nzuri zilizokuwa zikiibeba Tanzania na watu wake, lakini sasa nchi yetu inatajwa kwa majina mabaya maeneo mengi.

Ni wakati muafaka sasa serikali na vyombo vyake vyote vya ulinzi na usalama, kubuni mbinu mpya za kubaini, kukamata na kufikisha kwenye vyombo vyombo vya sheria wote wanaofanya vitendo hivyo haramu dhidi ya raia wa Tanzania.

Matukio haya yakizoeleka zaidi, huenda yakajenga mazingira ya hofu kwa wananchi kuhusu maisha yao, kwani kuifikia kesho, siyo tena majaaliwa na Mwenyezi Mungu, bali utashi wa “wasiojulikana.”

Mungu ibariki Tanzania na watu wake wote.

Katuni



Tunajali na kuthamini...



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ridhiwani Jakaya Kikwete akimvisha kofia pana mmoja wa watu wenye ualibino jijini Dodoma. Hafla ya kukabidhi vifaa kwa watu wenye ulemavu iliandaliwa na Ikupa Trust Fund. (Picha na Mpi-gapicha Wetu).

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi PAUL	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

Kimataifa

India, Pakistan wazidi 'kuchapana'

Na Mwandishi WETU

Uhasama kati ya India na Pakistan umekuwa mkubwa kiasi kuwa licha ya kutangaza kusitisha mapigano, lakini mapigano yamendelea baina yao.

Makubaliano ya kusitisha makubaliano yali-fikiwa juzi - Jumamosi, lakini ilipofika jana kila nchi ilikuwa ikilaumu nyingine kwa kukiuka makubaliano hayo kwa kuendeleza mashambulizi.

Hivi sasa nchi hizo zinakaribia kuanzisha vita kamili baina yao ambayo inaweza kuhusisha silaha za nyuklia.

Katika siku za hivi karibuni, kila upande umekuwa ukishambulia upande mwingine kwa kutumia ndege-nyuki (drone) na kusababisha madhara kwa binadamu na mali, huku zikien-delea kushutumiana kwa mashambulizi hayo.

Hali ya usalama baina ya nchi hizo mbili ilianza kuzorota baada ya kundi la Resistance Front (TRF) ambalo linaungwa mkono na kundi jingine ambalo India inaamini kuwa linaungwa mkono na Pakistan, kuishambulia India na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 20.

Kama sehemu ya kulipiza kisasi, India ikashambulia ngome ya kundi hilo katika eneo la Kashmir, ambalo linagombewa baina ya nchi hizo mbili.

Katika mashambulizi hayo, Pakistan ikadai kuwa maeneo yake mengine ya kiraia yame-shambuliwa, hivyo nayo ikaanzisha mashambulizi dhidi ya India kwa kutumia ndege-nyuki.

Machafuko ya sasa yamedumu kwa wiki kadhaa na kusababisha vifo vya mamia ya watu kila upande.

Wachambuzi wa masuala ya kiulinzi wanaona kuwa kuendelea kwa mgogoro huo, kuna-weza kuhatarisha amani katika Bara la Asia, hasa ikizingatiwa kuwa nchi hizo zina nguvu kubwa kijeshi, zote zikimiliki silaha kali za nyuklia.

Nchi nyingi duniani, zikiwamo Uingereza, Ufaransa na Urusi, zimeelezea wasiwasi kuhusiana na kukua kwa machafuko kati ya nchi hizo.

Jarida la Military Watch linaitaja India kuwa



moja kati ya nchi tano duniani kwa nguvu kubwa za kijeshi, huku Pakistan ikiwa ni ya tisa.

Kwa ujumla, India inaonekana kuwa na nguvu kijeshi kuliko Pakistan ikiwa na jeshi kubwa linaloundwa na silaha za kisasa.

Kwa upande wake, Pakistan inaelezwa kuwa na jeshi dogo, lakini lenye maarifa na ujasiri mkubwa.

Ingawa hakuna kati ya nchi hizo ambayo ime-wahi kutumia silaha za nyuklia katika mapigano awali, lakini kuna wasiwasi utamaduni huo siku moja unaweza kuvunjwa.

India ina vichwa vya mabomu ya nyuklia 180 huku Pakistan ikiwa na vichwa kama hivyo 170.

Ingawa India ina sera ambayo inaikataza kutumia silaha za nyuklia kwanza kwenye machafuko, lakini kumekuwa na taarifa kuwa imekuwa ikifikiria kubadili sera hiyo tangu 2019.

Pakistan haijawahi kuwa na sera ya aina hiyo, hivyo haina vikwazo vyovyote kwenye uamuzi wa kutumia silaha za nyuklia, huku ikidai kuwa matumizi ya kimkakati ya silaha hizo ni moja ya njia za kukabiliana na India.

Dunia: Hapa na Pale



Ujana wa Papa Leo

KAKA wa Papa Leo XIV, Louis Prevost amesema kuwa mdogo wake ambaye wiki iliyopita alichaguliwa kuwa Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani (RC), alikuwa na maisha ya utaua tangu akiwa mtoto.

Louis amesema familia yake ilikuwa ikimtabiria kuwa “kijana bora” zaidi kwa kuwa hakuwa na chembe ya ukorofi, alikuwa mpole na mwenye unyenyekevu tangu kuzaliwa kwake.

“Tabia na makuzi yake yalitustaajabisha, hakuwahi kufokewa na wazazi wetu na hata mimi, ambaye ni mkubwa sana kwake, sikuwahi kumnyooshea kidole kwa lolote, alikuwa mwema na mwenye hofu ya Mungu tangu uto-to wake,” amesema kaka yake huyo anayeishi Florida, Marekani.

Wakamia Ruto ang’oke

VITIMBI vya siasa, havilali. Sasa Seneta wa Kaunti ya Nairobi, Edwin Sifuna, amesema chama cha Orange Democratic Movement (ODM) cha Kenya, kimejipanga kumfanya Rais Wiliam Ruto kuwa rais wa muhula mmoja.

Sifuna, ambaye ni Katibu Mkuu wa ODM amesema kuwa chama hicho cha upinzani kina uhakika wa kushinda uchaguzi ujao na kuchukua uongozi kutoka kwa Rais Ruto kupitia uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2027.

Kiongozi huyo ambaye amekuwa akikosoa baadhi ya viongozi wa ODM kuwa na ushirikiano na serikali ya Ruto, amesema chama hicho kitakuwa na mgombea wa urais katika uchaguzi ujao ambaye ataishangaza dunia na siyo Kenya pekee kwa kuibuka mshindi.

Dau la bilioni 2/- lako

MAREKANI imetangaza zawadi ya dola milioni 10 (Shilingi bilioni 2.7) kwa yeyote atakayetoa habari au kufanikisha kukamatwa kwa mtuhumiwa wa ugaidi, Abdullahi Banati.

Banati anadaiwa kupanga shambulio la Januari 5, 2020 katika Kambi ya Jeshi ya Manda Bay, Kaunti ya Lamu, Kenya.

Marekani imemtaja Banati kuwa ni mwanachama wa kundi la ugaidi la Jaysh Ayman linalohusishwa na Al-Shaabab, ambalo limekuwa likitajwa kuhusika na matukio ya kigaidi.

Jaji mwanamke afungwa miaka sita

JAJI wa Umoja wa Mataifa, Lydia Mugambe (50), ambaye alikuwa akiishi Uingereza, amehukumiwa kifungo cha miaka sita na miezi minne jela, baada ya kupatikana na hatia ya kuajiri “dada wa kazi” bila kumlipa ujira wake.

Mugambe ambaye ni raia wa Uganda, alipatikana na hatia kwa makosa yakiwemo ya dhuluma kwa msichana wa kazi, kudanganya serikali kwamba alikuwa ndugu yake wakati akieleza sababu za kumpeleka Uingereza.

Inadaiwa kuwa jaji huyo alimfanya binti huyo kuwa mlezi wa watoto wake, kuan-galia nyumba yake na zaidi sana kuwa mp-ishi. Nafasi yake ya kuwa mtumishi wa Umoja wa Mataifa hai-kuwa kinga ya kutohu-kumiwa.



Habari Kuu

Wametishwa



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) - Dayosisi ya Karagwe, Askofu Benson Bagonza

Na Mwandishi WETU

VITISHO dhidi ya raia wa Tanzania wenye mawazo mbadala kushauri serikali vinazidi kushamiri.

Raia wamekuwa wakitishiwa kuumizwa na hata kuuawa kutoka kwa “watu wasiojulikana” – kwa kuwa tu wanakosoa baadhi ya mienendo ya utendaji wa serikali.

Wiki iliyopita pekee, watu watatu maarufu nchini, wamepokea vitisho dhidi ya maisha yao kutoka kwa kundi la watu hao.

Hawa ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) - Dayosisi ya Karagwe, Askofu Benson Bagonza, mwanasheria wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Wakiili Lugemeleza Nshala na Rais wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Wakili Boficafe Mwabukusi.

Watatu hao wamejitokeza hadharani kuelezea jinsi walivyopokea vitisho kutoka kwa watu wasiojulikana.

Viongozi hao wa taasisi kubwa nchini kwa

nyakati tofauti, wameliambia gazeti la Pambazuko kuwa wamepokea vitisho vya kuuawa na hatua ambazo wamezichukua.

Mbali na kuandika kwenye ukurasa wake wa X (zamani twitter), namba ya simu aliyo-dai imetumika kumtumia ujumbe wa vitisho vya kuuawa, Wakili Mwabukusi amesema amemtumia ujumbe huo Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mbeya (RCO), huku akisubiri Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kuchukua hatua kama wanavyofanya katika matukio ya watu wengine.

“Ni sahihi, nimekuwa nikipokea ujumbe tofauti wa vitisho, lakini huu wa leo (Jumamosi) nimeamua kuuweka hadharani na pia kumtumia RCO ili aufanyie kazi, na kamwe sintokubali kutishwa,” amesema Mwabukusi.

Askofu Bagonza na Dkt. Nshala, kwa nyakati tofauti wamesema kuwa hawajaripoti vitisho hivyo kwa Jeshi la Polisi isipokuwa wameamua kueleza umma na dunia juu ya hatari iliyo mbele yao.

Mbali na vitisho, Askofu Bagonza amesema amewahi kupokea vitisho zaidi ya mara moja na watu anaodhani wanajituma wenyewe ili kufurahisha watawala.

Amesema katika miaka ya karibuni aliwahi kunyang’anywa pasi ya kusafiria akiwa uwanja wa ndege na kuelezwa kuwa amezuiwa kutosafiri nje ya nchi.

Hata hivyo, baadaye aliruhusiwa kupanda ndege baada ya “wakubwa kuingilia kati.”

Kiongozi huyo wa dini ambaye amejizolea umaarufu mkubwa kutokana na aina ya ukosoaji wake, amesema wakati wa utawala wa serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli, aliwahi kuripoti mara kadhaa kwa vyombo vya usalama kuhusu kupokea vitisho mbalibali juu ya maisha yake, lakini hakuwahi kupewa mrejesho wa hatua zilizochukuliwa.

Amesema hata tukio la juzi hakuliripoti, lakini akaamua kuandika kwenye mitandao ya kijamii na ndipo alipofuatwa na vyombo vya dola kuzungumza naye.

“Safari hii sikuripoti, yawezekana nilikosea, lakini waliposoma niliyoandika walikuja, tuka-wa na mazungumzo mazuri...”

Inaendelea Uk. 7

Wametishwa

Inatoka Uk. 6

“Safari hii ni ya pili kuandika, mara ya kwanza ilikuwa Desemba 2020, hii ni mara ya pili na sababu kubwa ilikuwa ni baada ya kuona kila mtu analalamika...”

“Makamanda wa Polisi nchi nzima walikuwa wanatoa taarifa za uhalifu wa ‘wasiojulikana’, serikali inalalamika, wanaharakati wanalalamika. Kesi nyingine mpaka zimesahaulika...”

“Nikaona nami nilalamike kwani ipo siku ‘wasiojulikana’ watalalamika kama mimi,” amesema Dkt. Bagonza wakati akihojiwa na Pambazuko.

Askofu huyo ambaye ni mkosoaji mkubwa wa masuala ya kisiasa na kijamii, amesema ukosoaji wake siyo kwa watawala tu, bali hata kanisa analoliongoza, analikosoa.

“Mungu tu ndiye hakosolewi. Sijui nilianza lini. Nitaacha nitakapopoteza pumzi. Kukosoa kwa upendo, heshima, haki, na weledi ni hulka yangu. Hata mimi ninajikosoa, ndio maana najiona mpumbavu kufanya vitu visivyopendwa na watu...”

“Kuhusu utendai wa Jeshi la Polisi nilikwishasema kwamba wasiojulikana wana nguvu kuliko vyombo vyetu, hivyo ingewezekana katika uchaguzi mkuu ujao tuwachague hao kwani wana silaha, magari, pingu, sare, na uwezo mkubwa wa kukwepa dola na kupoteza watu,”

Dkt. Bagonza amesema.

Dkt. Bagonza anasimulia kwamba aliwahi kuonja shubiri ya ukosoaji wake - kwa mara ya kwanza mwaka 1976, wakati huo akisoma darasa la sita.

Akisimulia kisa hicho, anasema alisimamishwa masomo kwa kipindi cha mwaka mzima kwa kitendo chake cha kuwakosa baadhi ya walimu waliokuwa na tabia ya kuwanyanyasa wanafunzi.

Amesema alirejea masomoni baada ya ofisa elimu wa mkoa kuamuru arudishwe shuleni.

Nshala amwachia Mungu

Dkt. Nshala, ambaye ni wakili na mwanaharakati maarufu nchini, amesema alipata ta-

arifa kutoka kwa watu wake wa karibu kuwa ni miongoni mwa watu wanaolengwa kuuawa.

Hata hivyo, hakuweka wazi ni watu gani wanaotishia uhai wake na wala hakutaja sababu za kuwindwa.

“Ni kweli juzi (Alhamisi) nilipokea taarifa kwamba mimi ni kati ya watu wanaowindwa...”

“Sababu kubwa ni kwamba niko karibu sana na Katibu wa Baraza la Maaskofu Katoliki nchini, Padre Dkt. Charles Kitima pamoja na kuwa kwangu mwanasheria mkuu wa Chadema...”

“Matishio (sahihi vitisho) ni mengi tangu mwaka 2022 na 2023, sipuuzii hizo taarifa, lakini mimi ni mtu wa imani, naamini Mungu yupo. Wale wanaopanga, kudhuru uhai wangu, damu yangu, itateketeza familia zao na vizazi vyao 440 vilivyopo na vijavyo,” amesema Dkt. Nshala.

Kuhusu kuripoti vitisho hivyo kwa Jeshi la Polisi, Dkt. Nshala amesema alitegemea baada ya taarifa kuwekwa mitandaoni, vyombo vina-nyohusika vimuite atoe maelezo, lakini havijafanya hivyo.

Msemaji wa Jeshi la Polisi Tanzania, David Misime, hakupatikana kutolea kauli suala hilo kwani simu yake ya kiganjani iliita bila kupokewa, lakini baadaye aliandika akitaka atumiwe ujumbe wa simu.

Hata hivyo, licha ya kutumiwa maswali hakuyajibu mpaka wakati habari hii inachapishwa.



Katibu TEC, Padre Dkt. Charles Kitima

Habari**Pambazuko lafanikisha fedha kurejeshwa**

Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kagera, Hajinas Onesphory, akimkabidhi fedha, Praxseda Benjamin (kulia) Mkazi wa Kijiji cha Bulembo, Tarafa ya Kamachumu wilayani Muleba, aliyetapeliwa fedha na wafanyakazi wa kampuni iliyopewa tenda ya kusambaza umeme, mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu)

Na Arodia PETER

GAZETI la Pambazuko limefanya kazi yake. Limewezesha wananchi tisa kurejeshewa fedha zao baada ya kutapeliwa.

Hatua hiyo imefanikiwa baada ya habari iliyoandikwa na gazeti hili, kufika kwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Kagera, na kuamua kufuatilia kwa uchunguzi zaidi.

Takukuru iliwafikisha watuhumiwa mahakamani na kuhukumuwa, huku wakiamuriwa kurejesha fedha.

Watuhumiwa hao walikuwa wafanyakazi wa Kampuni ya Nakuroi Investment, ambayo ilipewa kandarasi ya kusambaza umeme vijijini.

Kampuni hiyo ilipewa zabuni ya kuunganisha umeme katika Kijiji cha Bulembo wilayani Muleba mkoani humo.

Kaimu Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Kagera, Hajinas Onesphory, Ijumaa iliyopita - Aprili 9, 2025 alikabidhi fedha hizo – kiasi cha shilingi 2,300,000 kwa wanakijiji tisa.

Kashfa wananchi hao kutapeliwa iliibuliwa na gazeti la Pambazuko kwa mara ya kwanza katika toleo la Januari 20 -26 mwaka huu kupitia habari hii; Umeme REA wageuzwa 'shamba la bibi.'

Baadaye Takukuru walifanya uchunguzi wa kina na kubaini ukweli wa kile kilichoandikwa na Pambazuko.

zuko.

Takukuru ikawakamata watuhumiwa na kuwafikisha mahakamani ambako walikutwa na hatia.

Watumishi hao waliwalazimisha wananchi kuchanga fedha ili kununua nguzo za umeme kati ka mradi unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) kijijini hapo, jambo ambalo ni kinyume na utaratibu kwani wananchi wanaounganishiwa umeme hawapaswi kuchangia gharama za nguzo.

Kupitia Pambazuko, wananchi hao walilalamika kutounganishiwa umeme licha ya kulipa fedha ambazo ziliishia kwenye mifuko ya watumishi hao.

Akizungumza wakati wa kukabidhi fedha hizo, Onesphory alisema baada ya taasisi yake kupata taarifa hizo, uchunguzi ulifanyika na watuhumiwa wawili walifikishwa mahakamani kwa makosa ya rushwa na kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu.

"Mahakama ya Wilaya ya Muleba baada ya kusikiliza shauri hilo mbele ya Hakimu Mfawidhi wa Mahakama, Daniel Nyamkyelya, iliwatia hatiani washtakiwa hao kwa makosa ya udanganyifu, ambapo pamoja na adhabu nyingine, Hakimu aliamuru fedha zote shilingi 2,300,000 zilizochukuliwa na Patrick Muchunguzi na Revocatus Masanja, kurejeshwa kwa wananchi husika kupitia ofisi ya Takukuru.

Mmoja wa wananchi hao, Akwilina Philemon alishukuru gazeti la Pambazuko lililoibua kashfa hiyo na baadaye Takukuru kuchukua hatua hadi kurudishiwa fedha zao. "Wenzetu hawaamini kama hili limeweze kana, tunashukuru sana chombo cha habari – gazeti la Pambazuko, kuibua jambo hili pamoja na Takukuru kwa kuturudishia furaha," alisema Akwilina.

Katika hatua nyingine, Takukuru Mkoa wa Kagera imezuia upotevu wa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 50 katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Missenyi.

Kaimu mkuu wa taasisi hiyo amesema baada ya uchunguzi walibaini kutokuwasilisha wala kutumika kwa vigae vyenye thamani ya shilingi milioni 50 huku nyaraka zote za manunuzi na mapokezi zikionesha kuwa vifaa hivyo vimenunuliwa na kupokewa kwenye eneo la mradi.

"Hadi sasa mzabuni amevirejesha na vimetumika kama ilivyokusudiwa na hatua dhidi ya watuhumiwa zitachukuliwa pindi uchunguzi utakapokamilika," alisisitiza Onesphory.



Waliokuwa viongozi wa Chadema wakionyesha mshikamano wao baada ya kutangaza kujiondoa ndani ya chama hicho wakati wa mkutano wao na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Picha na Fidelis Felix

Wananchi waombwa kuamini Polisi

Na Rachel MRISHO

WANANCHI wametakiwa kuhakikisha wanaliamini Jeshi la Polisi na kulipa ushirikiano ili lifanye kazi zake kwa ufasaha.

Mkuu wa Kituo cha Polisi Madale, jijini Dar es Salaam, Mrakibu wa Polisi Japhet Mgonja, ameeleza hayo hivi karibuni kwenye mkutano wa wananchi wa Kata ya Wazo Hill, ambapo mbali na mambo mengine, ulijadili suala la ulinzi wa raia na mali zao.

“Amani ya nchi inajengwa kuanzia kwenye familia zetu, ulinzi na usalama uchukuliwe kama mtaji wetu...”

“Jamii inatakiwa kutambua umuhimu wa ulinzi shirikishi kwani unasaidia kupunguza uhalifu na kusambaratisha magenge ya wahalifu.

“Mahali popote ambapo jamii inatoa ushirikiano katika ulinzi huwezi kusikia kuna matukio ya kihalifu ya mara kwa mara, sasa nasema hivi kila mkazi lazima ashiriki kikamilifu katika ulinzi...”

“Ambaye haelewi ulinzi shirikishi, aje kituoni tutamueleweshe na kumuelimisha, msilogope Kituo cha Madale mmekijenga wenyewe...”

“Huko mitaani kuna matukio mengi ya kikatili. Watoto na akina mama wananyanyasika, toeni taarifa na muamini jeshi lenu...”

“Pia kuna watu wanahamasisha uvunjifu wa amani, ndugu zangu mjue kuwa kama amani haipo na maendeleo hayatakuwepo...”

“Nawasihi msiwe na mihemko kwenye mambo yenye viashiria ovu,” amesema Afande Mgonja.

Aidha, ametoa mwito kwa wananchi kuen-delea kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa mapema kwenye vyombo vya usalama, endapo kuna viashiria vya uvunjifu wa amani na ukatili wa kijinsia.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyakasangwe, Zuhura Mabewa, amesema kwa kuwa suala la ulinzi shirikishi lipo kisheria, kila mwananchi anapaswa kuchangia fedha kwa ajili ya kuwalipa vijana wanaojitolea kulinda kwenye maeneo wanayoishi.

Mkazi wa eneo la Msigani, Josephat Zakayo, amesema ili jamii ijenge imani na walinda amani wakiwamo polisi, siasa isihusishwe.

“Hakuna mtu anayependa kuishi bila amani, polisi wetu wasihusike kwenye siasa, wafanye kazi ya kutulinda na hawa polisi jamii wafanye kazi kwa kuzingatia sheria na kanuni zina-vyowaongoza,” ameshauri Zakayo.

Mhamasishaji wa Vikundi vya Ulinzi Shirikishi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, Emmanuel Malila, amesema vikundi vingi vya ulinzi shirikishi vinakufa kwa sababu ya viongozi wa mitaa wanaingiza masuala ya siasa.

“Walinzi shirikishi hawachagui hali ya kipato. Kama wananchi wamekubaliana kiwango cha kulipa, kila mtu alipe hata kama unalala kwenye boksi au nyumba yenye geti na mbwa wote walipe,” amesema.

Tafakuri ya BagonzaNa Dkt. Benson
BAGONZA

Kama ni kweli wamekosea, kama siyo wamekosea pia

MEI 8, mwaka huu – 2025, ni siku ambayo Papa wa 267 (Papa Leo XIV) alichaguliwa.

Huyu ni mwana Chicago mwenzangu; mwana Catholic Theological Union (CTU) mwenzangu, na mwana Augustino mwenzangu (Msisahau Luther alikuwa Augustinianian).

Pamoja na tukio hilo la kupatikana kiongozi mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, kwangu ilikuwa siku njema na ngumu.

Ngumu kwa kuwa nimekuwa napokea taarifa na tahadhari kuwa “wasiojulikana” watakuja kunimaliza.

Sishangai maana ukimfuga mbwa ukamwachia aonje damu za watu, huwezi kumdhibiti tena na hawezi kuacha mwenyewe.

Sasa basi, kama ni kweli wanakuja; wameko-

sea. Wanaichafua serikali na taifa kwa jumla.

Kama siyo kweli, pia wamekosea. Wanaichafua serikali na taifa letu pendwa hata kwa kuwaza hayo.

Kama wakija, nawaomba wasiharibu milan-go ya nyumba yangu kuwafanya yatima kuitengeneza upya. Waniite, nitatoka nijikabidhi.

Kama hawapo na kwa hiyo hawaji; nashauri kama nilivyomshauri mfuga mbwa kuwa awafungie mbwa wake ndani. Siyo kwa ajili yangu, bali kwa ajili ya mfunga mbwa na kijiji chetu.

Huu ni mwaka wa uchaguzi. Hekima ni kutengeneza marafiki wapya kuliko maadui wapya. Usimuue anayetaka kufa. Ni matumizi mabaya ya mauaji.

Niwakumbushe machache haya.

Katika awamu ya tano walikuja. Siyo lazima waje awamu ya sita, hata kama awamu ya sita ni muendelezo wa awamu ya tano!

Iwe awamu ile au hii, hawa wasiojulikana ni waharibifu wa awamu zote mbili. Serikali maki-ni, na hii ni makini, kama haiwajui, ijitenge nao siyo kutujulisha kuwa wapo.

Hawa wasiojulikana wanaweza kufanya kwa sababu wameishafanya pasipotegemewa. Waki-fanya, wasijipongeze, wasipongezwe, na adhabu yao iwe ni kufanya milele.

Kama wakifanya; mwili utaoza, watu watalia na wengine watashangilia, lakini, ukweli hautazikwa, upumbavu wangu hautazikwa na watazaliwa wapumbavu wengine zaidi yangu.

Mungu analipenda taifa hili kuliko ninavyo-lipenda. Hachelewi wala hawahi. Atasimama kulitetea.

Naishi katika jimbo la Waziri wa Mambo ya Ndani. Nina uhakika hakuwatuma. Nawashauri wasitumie rungu kuua mbu aliyekaa makende ya mfalme. Watamuumiza. Watumie hekima, mbu ataondoka.

Wasimtungue kwa jiwe la manati kunguru mchafu aliyekaa juu ya kichwa cha malkia. Wakikosea kidogo, jiwe litamjeruhi malkia.

Nawapenda Watanzania. Tusipoonana tena, tutakutana kwa Baba wale mlio na imani.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.

Papa Leo
XIV

Na Godwin CHILEWA,
Houston



Kurunzi la Intelejensia



Bunge lisimame kwenye haki, kweli

BUNGE ni chombo muhimu katika kuwakilisha wananchi, kutunga sheria, na kusimamia serikali.

Hivyo basi, linapaswa kuwa sauti ya ukweli, ulinzi wa haki, na dira ya utawala bora. Kwa bahati mbaya Bunge letu sasa ni kama linea tunu hizo na kugeuka kuwa chombo cha mhimili mwingine wa utawala; serikali.

Hivi karibuni, Bunge la Ulaya lilijadili hali ya kisiasa nchini Tanzania likibainisha ukiukwaji wa haki za binadamu, kuteswa kwa wapinzani, na matumizi mabaya ya sheria kama njia ya kuwakandamiza viongozi wa upinzani, akiwemo Tundu Lissu.

Hili lilipaswa kuwa fursa kwa Bunge la Tanzania kutathmini ukweli wa mambo na kuchukua hatua kulinda katiba, badala ya kujihami kwa kejeli na kuhamisha mjadala kutoka ajenda kuu na kusimamia hoja ya ushoga.

Ni kweli kwamba ushoga ni dhambi ya Sodoma na kinyume cha maadili ya Kiafrika. Hata hivyo, badala ya kukiri changamoto na kushughulikia madai ya ukandamizaji wa vyama vya upinzani, utekaji nyara, na kesi zenye kubeba

dalili za uonevu, wabunge wetu kwa makusudi walihamishia mjadala kwenye hoja ya ushoga, na kuifanya kuwa ajenda kuu ya majibu yao.

Jambo hili lilifanywa makusudi ikiwa njia ya kupotosha umma na kufunika hoja nzito za kisiasa zinazohusu demokrasia, uhuru wa maoni, na haki ya kuchagua viongozi bila vitisho.

Huu ni usaliti kwa wananchi.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua haki za binadamu, uhuru wa kisiasa, na uwajibikaji wa serikali kwa wananchi.

Bunge linapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha haki hizi zinalindwa bila upendeleo wala itikadi.

Kukwepa hoja za msingi kwa kutumia mihemko ya kisiasa ni kutowatendea vyema wananchi wa Tanzania.

Ni wakati sasa kwa Bunge la Tanzania kusiama juu ya misingi ya ukweli na haki.

Wabunge wanapaswa kutumia nafasi yao kuhimiza utawala wa sheria, kuheshimu katiba, na kutetea uhuru wa vyama vyote vya siasa.

Kupinga ukandamizaji siyo sawa na kupokea maagizo ya kigeni; ni kutimiza wajibu wa kizalendo kwa mustakabali bora wa taifa.

Wazo Binafsi

Tutegemee nini kupitia Kaulimbiu ya Papa Leo?

Na Askofu Severine NIWEMUGIZI

KAULIMBIU ya Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani (RC), Papa Leo XIV ni; “In Illo Uno Unum,” yaani - “Katika Mmoja Tuko Wamoja.”

Papa Leo XIV ameeleza katika mahojiano akionyesha mwelekeo wa kuwaza kwake na utendaji wake utakakoelekea.

Akifafanua kaulimbiu yake amesema; “Kama inavyoonekana kutoka kwa kaulimbiu yangu ya kiaskofu; umoja na ushirika kwa kweli ni sehemu ya karama ya Shirika la Mtakatifu Augustino, na pia njia yangu ya kutenda na kufikiri.”

Akaongeza; “Ninaamini ni muhimu sana kukuza ushirika katika Kanisa, na tunajua vyeema kwamba ushirika, ushiriki, na utume, ni maneno matatu muhimu ya Sinodi. Kwa hiyo, kama Muagustiniani, kwangu kukuza umoja na ushirika ni jambo la msingi.”

Pamoja na mwelekeo wa kukuza umoja kuna mambo kadhaa mengine tunaweza kuyategemea pia.

Moyo kwa masikini

Papa Leo XIV ametumia muda mwingi wa ukuhani wake katika baadhi ya maeneo yaliyo-sahaulika zaidi duniani, makazi duni, maeneo ya vita, na kambi za wakimbizi.

Yeye anahubiri tu juu ya maskini; anatembea nao na kuomba pamoja nao. Atakuwa mwendelezaji wa sauti ya Papa Francis kuwatetea masikini wa dunia wasisahaulike.

Mwanzo mnyenyekevu

Alizaliwa katika kijiji tulivu. Maisha yake yalianza kwa urahisi, familia yake haikuwa tajiri, lakini walikuwa matajiri wa imani. Mara nyingi alisema; “Ni bibi yangu ambaye alinifundisha kwanza jinsi ya kuzungumza na Mungu.

“Bila shaka ana nguvu kubwa ya kumsikiliza Roho Mtakatifu.

Mungu amependa kwa changamoto za nyakati hizi amtumie kuisikiliza sauti yake Roho wa



Papa Leo XIV

Mungu na kuishauri dunia twende njia ipi salaama.

Yeye ni “polyglot”

Papa huyu anazungumza lugha saba kwa ufasaha, na siyo kwa ajili ya maonyesho tu. Anazitumia kuvunja vizuizi na kuwafanya watu wajisikie kuonekana, haijalishi wanatoka wapi.

Sauti ya ujasiri katika msiba

Wakati wa ghasia katika nchi yake, alihatarisha maisha yake kwa kuwahifadhi watu walioteswa ndani ya kanisa lake la parokia.

Haogopi kusimama motoni kwa ajili ya ukweli wala haogopi kutetea imani yake.

Naamini amekuja muda mwafaka tunapokuwa na uhasama wa mataifa pande mbalimbali za dunia; watu wakiteseka kwa sababu za vita na ukandamizwaji wa haki zikiwamo za uhuru wa kuabudu na demokrasia, naamini atatoa sauti ya kinabii bila woga.

Siyo shabiki wa kung'ara

Kama vile Papa Francisko, usitarajie pete za dhahabu na viingilio vikubwa.

Leo XIV anapendelea viatu vilivyovaliwa kuliko viatu vilivyosafishwa na mara moja alitoa msalaba wake wa kiaskofu kwa mtu asiye na makazi.

Ni mwana wa Maria

Kujitolea kwake kwa Mama Yetu Bikira Maria kunashangaza. Anaanza kila siku na Rozari na kuimaliza mbele ya picha ya Mariamu aliyobeba tangu akiwa seminari.

Bila shaka anatumiza nasi kumkimbilia Mama atuombee tuwapo kwenye changamoto kubwa za maisha.

Wakili wa vijana

Anaamini Kanisa haliwezi tu kuzungumza na vijana, ni lazima liwasikilize. Wakati fulani alifanya mkesha wa usiku kucha ili tu kujibu maswali kutoka kwa kundi la wanafunzi wa chuo kikuu.

Mwandishi ni Askofu wa Jimbo Katoliki la Ruenge.

Gambo azidi kumparura Makonda



Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo

Na Rachel MRISHO

MSUGUANO baina ya Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, wachukua sura mpya.

Sasa Gambo ameanza “kufunguka” na kuweka siri hadharani – kwamba Makonda “aliumiza sana watu.”

Akizungumza juzi katika mkutano wa hadhara aliouandaa jijini Arusha, Gambo alisema kuwa ana tuhuma nzito dhidi ya Makonda.

Mbunge huyo alisema yapo mambo mengi ambayo hakuwa tayari kuyaweka wazi, lakini amelazimika kuyasema hadharani badhi ili jamii ifahamu ukweli.

“Kuna mambo mengine sikutaka kuyasema kwa sababu nina uwezo mkubwa wa kupuuza, lakini nimechokonolewa sana na baadhi ya watu, kiasi ambacho inawezekana kuna watu wengine mkachanganywa...”

“Kwa sababu nimelazimishwa, lakini mengi nimeyapuuza, lakini nitasema angalau moja, naomba mnikubalie...”

“Leo amediriki kusimama na kusema eti Gambo ameumiza watu wengi, hivi nataka niwaulize mimi na yeye nani amewaumiza watu

wengi zaidi katika nchi hii?” Alihoji Gambo.

“Nyie mnaokujua Dar es Salaam? Nendeni mkatafute habari zake kule mkizipata hata kum-salimia mtaogopa...”

“Nataka alipo kokote mwambieni mikononyangu ni safi, sina changamoto yoyote, sijamuumiza yeyote na badala yake, nimesaidia watu wengi sana kote nilikopita kwenye uongozi wangu,” alisema mbunge huyo.

Ingawa hakutaja jina, lakini kwa yale yanayoendeela katika siku za hivi karibuni kuhusiana na siasa za Arusha Mjini, yanayonyesha wazi kuwa alikuwa anamlenga Makonda.

Hata hivyo, Gambo hakutaja walioumizwa wala njia zilizotumika kufanya hivyo.

Kabla ya kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Makonda aliwahi pia kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mbunge huyo alirudia kauli yake kuhusu kuwepo kwa ubadhirifu wa fedha za jengo la utawala la mkoa na kusema; “jengo la utawala linatakiwa kuwa la ghorofa nane, awamu ya kwanza ground floor (ghorofa ya chini) wame-lipa (shilingi) bilioni 1.81, wakamaliza wakatangaza tenda wakapata mkandarasi kwa (shilingi) bilioni 11. Jumla ni zaidi ya (shilingi) bilioni 12...”

“Ukigawanya kwa nane kila ghorofa moja sawa limejengwa kwa shilingi bilioni 1.58 hii haikubaliki, ni wizi...”

“Baadaye wakaingia mkataba mdogo wa shilingi bilion 6.2, nikapata taarifa kuwa kuna mtu badala ya kuandika square meter (meta ya mraba) ameandika cubic meter (meta ya ujazo) huu ni wizi kwa kufanya hivyo wameongeza shilingi bilioni 1.8...”

“Mimi nilitegemea niugwe mkono badala yake nakwenda kudhalilishwa hadharani. Kama walikuwa hawataki niongee, wangemchukulia hatua kwa sababu kile kitendo alichokifanya hakina utu, lengo lake lilikuwa ni kunitisha...”

“Nataka atoke hadharani aseme kama nimeongea uongo, kazi ya mbunge siyo kuimba mapambio,” alisema Gambo.

Habari

ACT yaibua mazito deni la taifa



Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Bara, Isihaka Mchinjita akichambua ripoti ya CAG kwa mwaka wa fedha 2023/24 jijini Dar es Saalam juzi.

Na Mwandishi WETU

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimebainisha hoja nyingi zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika ripoti yake ya mwaka 2023/24, kikisema ubadhirifu wa fedha za umma umekuwa ukijirudia mwaka hadi mwaka.

Baada ya kusoma na kuchambua ripoti hiyo, chama hicho kinaeleza kuwa kimebaini mambo kumi ambayo yanatakiwa kuchukuliwa hatua za haraka.

Moja kati ya maeneo hayo ni pamoja na hatari ya kasi ya kuongezeka kwa Deni la Taifa, ambapo limepanda hadi kufikia shilingi trilioni 97.35 kutoka shilingi trilioni 82.25.

Kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu, amesema hayo juzi - Mei 10, 2025 jijini Dar es Salaam alipotoa uchambuzi wa ripoti ya CAG.

“Ongezeko hili la Deni la Taifa ni zaidi ya shilingi trilioni 15 kwa mwaka mmoja pekee. Hali hii inaweka hatari mustakabali wa taifa kwani baadhi ya viashiria kama ‘uwiano wa kulipa deni kwa mapato’ vinakaribia ukomo wa hatari uliowekwa na taasisi za kimataifa,” amesema.

Amesema serikali imekopa shilingi trilioni

33.18 ikijumuisha shilingi trilioni 17.7 ambayo ni mtaji huku shilingi trilioni 9.48 ikiwa ni riba.

“CAG ameonesha kuwa uwiano wa kulipa deni kwa mapato ya ndani umefikia asilimia 14.5, ukikaribia kikomo cha tahadhari cha asilimia 18...”

“Aidha, uwiano wa kulipa deni kwa mauzo ya nje ni asilimia 11.7, ukielekea ukomo wa hatari wa asilimia 15,” amesema Semu.

Kutokana na hilo, amesema sehemu kubwa ya mapato ya serikali inaishia kulipa madeni badala ya kuendeleza huduma kwa wananchi.

“Mapato ya serikali kwa Januari 2025, kwa mfano ilikusanya shilingi trilioni 2.63 katika makusanyo hayo, serikali ilitumia shilingi trilioni 1.2 kulipia huduma ya deni...”

“Uchambuzi wetu unaonesha kuwa Serikali ya Tanzania inalipa kati ya shilingi bilioni 900 hadi trilioni 1.3 kwa mwezi kwa ajili ya huduma za deni...”

Hii inaonyesha mzigo mkubwa wa deni kwa serikali, ambao unaathiri uwezo wa kutoa huduma muhimu kwa wananchi kama afya, elimu na miundombinu,” amesema.

Akichambua kuhusu matumizi ya serikali kwa mwaka 2023/24, Semu amesema unaonyesha kuwa fedha za makusanyo ya ndani yalikuwa shilingi trilioni 29.99.

Akichanganua hilo, amesema mgawanyo wa matumizi ni kuwa shilingi trilioni 10.35 zilitumika kwa ajili ya kulipa mishahara, shilingi trilioni 18, zilitumika kuhudumia deni la serikali na matumizi mengineyo.

Kuhusu miradi ya maendeleo, kiongozi huyo amesema serikali ilipangiwa shilingi trilioni 15.1 ambayo yote ilitegemea mikopo.

“Yaani kila shilingi 100 inayokusanywa, shilingi 65 inaenda kulipia mshahara wa rais na watu wake, posho, masurufu na chai huku shilingi 35 ndiyo inawekezwa kwa maendeleo ambayo yote inategemea mikopo...”

“Ndiyo maana wananchi wakiuliza maswali kuhusu deni, serikali imekuwa ikijitetea kuwa deni ni himilivu, maana yake wao ndiyo wana-nufaika,” amesema.

Inaendelea Uk. 15

ACT yaibua mazito...

Inatoka Uk. 14

Alitahadharisha kuwa athari za mzigo huo wa madeni ni kubwa kwa wananchi wa kawaida kwa sababu ni fedha ambazo zilipaswa kujenga shule, hospitali, maji safi na barabara zinamezwa na kulipa riba ya madeni.

Vilevile amesema katika uchambuzi wao, wameonesha ubadhirifu wa fedha za umma katika utekelezaji wa miradi na majukumu mbalimbali ya wizara, taasisi za serikali na mashirika ya umma, bila kuchukuliwa hatua za uwajibikaji.

Kutokana na hilo, chama hicho kimeitaka serikali kuacha kuhadaa wananchi kuhusiana na hali halisi ya Deni la Taifa, kwani halitoshi kutazamwa katika jicho la kiuchumi wa jumla pasipo kuangalia hoja za kina siasa-uchumi na kijamii.

“Serikali inapaswa kuchukua hatua madhubuti kuhakikisha ufanisi katika makusanyo ya ndani, ili kujiwekeza zaidi katika uchumi unaojitegemea.

Serikali inapaswa kuzingatia mipango yake na kujiepusha na mienendo ya ulafi wa mikopo isiyokuwa na mipangilio,” amesisitiza.

Kuhusu madai ya wazabuni na wakandarasi yenye thamani ya shilingi trilioni 4.5, Semu amesema madai hayo sasa limekuwa tatizo sugu.

“CAG amebaini serikali kuwa na madai yasiyolipwa ya shilingi trilioni 4.56, ambapo shilingi trilioni 3.53 hazijalipwa kwa zaidi ya mwaka mmoja.

Hiki ni kiwango kikubwa sana cha fedha za watu ambazo serikali inazishikilia mkononi, baada ya kupokea huduma za wazabuni hao,” amesema.

Amesema kwa mwaka 2023/24 pekee, serikali imesababisha wakandarasi kudai riba ya zaidi ya shilingi bilioni 55.55, fedha ambazo zingetumika kwa huduma muhimu kwa wananchi kama afya, elimu na maji.

Vilevile, kushindwa kwa serikali kulipa madeni ya wakandarasi na watoa huduma kumechangia kudorora kwa kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa

barabara, hospitali, shule na miundombinu ya maji.

“Ndiyo maana tunaona barabara maeneo mbalimbali nchini zimesimama, hakuna ujenzi unaendele), hazifanyiwi matengenezo, ukarabati au kuendelea kujengwa, mathalan Barabara ya Rufiji – Mtwara,” amesema.

Pamoja na kumulika na kuainisha ubadhirifu na upotevu wa fedha, ACT-Wazalendo kimesisitiza watumishi wote wanaohusika na kuwezesha kuwepo, na kushamiri kwa vitendo vya ubadhirifu na upotevu wa mapato, wakamatwe na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Chama hicho kimevitaka vyombo vya habari kutekeleza wajibu wao wa kiukombozi kuangazia, kumulika na kuweka hadharani vitendo vya ubadhirifu na upotevu wa mapato.

“Tunasisitiza kwamba serikali ihakikishe kwamba mfumo wake wa kielektroniki unafanya kazi kwa wakati wote na maeneo yote na kuweka utaratibu wa kutokuruhusu miamala kufanyika nje ya mifumo hiyo.

“ACT-Wazalendo tunatamka kwamba hatuwezi kuendelea kukaa tu na kubaki kuwa mashuhuda, wakati fedha za umma zinaliwa, miradi ya maendeleo inatelekezwa na Watanzania wanaumia na kuteketea,” amesema.



Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu akichambua ripoti ya CAG kwa mwaka wa fedha 2023/24 jijini Dar es Saalam juzi.

Habari

Mitambo kusafishia Ziwa Victoria yaja

Na Mwandishi WETU, Mwanza

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, amesema serikali ipo hatua za mwisho kununua mitambo mitatu ya kisasa kwa ajili ya kukomesha magugu maji katika Ziwa Victoria.

Mtanda amesema mitambo hiyo itatumika kusafishia magugu maji ambayo yageuka changamoto kubwa katika ziwa hilo.

Mara kadhaa vivuko katika kivuko cha Kigongo-Busisi vimelazimika kusitisha safari zake baada ya kuharibika kutokana na kuongezeka kwa magugu maji katika aneo hilo.

Mtanda amesema hayo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa ziara ya ukaguzi wa zoezi la udhibiti wa magugu maji.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kusikia kilio cha wananchi wa Jiji la Mwanza kuhusu changamoto hiyo.

“Hapa tuna feri tatu, lakini baada ya ujio wa magugu maji, hasa yale madogo madogo ambayo tayari tumeanza kuyavuna yalikwamisha feri zetu na sasa tunatumia shilingi milioni mbili kwa siku kwa ajili ya usafi...”

“Msitu unaoonekana ndani ya ziwa ni athari zenyewe za magugu maji na kufanya kukwamisha kazi zetu za kila siku tunazofanya, hivyo habari njema ni kwamba Rais Samia amesikia kilio chetu,” amesema Mtanda.

Hata hivyo, Mtanda hakueleza mitambo hiyo imenunuliwa kutoka wapi au itawasili lini nchini.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Lehemaja, amesema magugu maji yanaleta athari kubwa ya mazingira, uchu-mi na kijamii, ikiwemo kuathiri viumbe hai vinavyoishi kwenye maji.

“Changamoto kubwa ni magugu yale ya zamani ambayo yanahitaji nguvu ya ziada na tayari tumeanza zoezi la kukabiliana nayo kwa kuyakata ili kuona spidi (kasi) ya kukua inapungua na hatua ya pili ni kununua mashine ya kisasa kama ambavyo ilivyoelekezwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa,” amesema Luhemeja.

Ameongeza kuwa changamoto bado ipo sababu magugu maji yanakua kwa haraka, lakini kwa kushirikiana na serikali ya mkoa, changamoto hiyo itadhibitiwa na malalamiko yaliyokuwepo tayari yameondoka.

“Kikubwa tunaendelea kuweka usafi na kufanya ziwa linakuwa salama na kuendelea na matumizi kama awali na wananchi wataendelea na shughuli zao bila changamoto yoyote,” ameongeza.

Hadi Mei 10, 2025 zaidi ya tani 600 ya magugu maji zilikuwa zimeondolewa katika Ziwa Victoria, huku zoezi hilo likiwa endelevu kwa ajili ya kukabiliana na magugu maji hayo yanayoharibu uhifadhi na utunzaji wa mazingira.



Baadhi ya vibarua wakitoa magugu maji ndani ya Ziwa Victoria katika zoezi linaloendelea eneo la Kivuko cha Kogongo-Busisi (Picha na Mpigapicha Maalum).

Mwabukusi aapa kumsaka Mdude

Na Hellen NGOROMERA

RAIS wa Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, ameapa kulivalia njuga suala la kupotea kwa kada maarufu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mpaluka Nyagali, almaarufu Mdude.

Akizungumza wiki iliyopita, Mwabukusi amesema wakati wowote kuanzia sasa atakwenda kuweka kambi mkoani Mbeya na kuongoza harakati za kushinikiza mamlaka zimtafute kijana huyo aliyepotea baada ya kuvamiwa na watu usiku akiwa nyumbani kwake.

Mke wa mwanaharakati huyo, amesema watu hao waliojitambulisha kuwa askari polisi na walivunja mlango na kuondoka na mume wake kwa nguvu.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi limekanusha kutuma watu kumkamata Mdude.

Mwabukusi ameendela kutuhumu Polisi kwa kupotea kwa Mdude akisisitiza kuwa haku-na raia wa kawaida anayeweza kumteka Mdude.

“Wiki hii nina kazi naimalizia na nikishaikamilisha, nitarudi hapa Mbeya na kuweka kambi kushinikiza Mdude apatikane na tunataka apatikane akiwa hai,” alisema kwa msisitizo.

Takribani wiki mbili sasa tangu Mdude apotee na hakuna taarifa zozote kuhusu alipo kijana huyo.

Makao Makuu ya Jeshi la Polisi limetuma timu ya wachunguzi kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya kufuatilia suala hilo.

Timu hiyo ina kazi ya kufuatilia tuhuma zilizotolewa na mwananchi mmoja kuwa siku



Mdude ni rafiki yangu nimemfahamu kwa miaka15. Hadaiwi, hagombani na mtu na wala hakopi kwa mtu. Adui wa Mdude ni mtu mmoja tu! Ni mtu asiyependa kukosolewa,” alisema Mwabukusi.

chache kabla Mdude hajatekwa, askari polisi mmoja alimtaka ashirikiane naye kumpoteza kijana huyo na kuwa akisaidia atalipwa fedha.

Jeshi la Polisi mkoani Mbeya nao wametangaza kuendelea na upelelezi na harakati za kumsaka Mdude.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, naye ameahidi kulipa shilingi milioni tano kwa mtu yeyote atakayefanikisha kupatikana kwa Mdude akiwa hai au amekufa.

Lakini Mwabukusi anasisitiza kinachotakiwa ni Mdude kupatikana akiwa hai.

“Kitu chochote kitakachotusimamisha kumtafute Mdude ni mauti,” anasisitiza Mwabukusi.

Kupotea kwa Mdude kumesababisha malalamiko na kuongeza kwa lawama kutoka kwa wananchi na wanaharakati ambao wamekuwa wakishinikiza mamlaka zimtafute Mdude hadi kumpata.

Siku chache baada ya kupotea, wananchi waliungana na majirani na rafiki wa Mdude kumtafuta katika viunga vya Jiji la Mbeya.

Hata hivyo, msako huo haukuzaa matunda.

“Mdude ni rafiki yangu nimemfahamu kwa miaka15. Hadaiwi, hagombani na mtu na wala hakopi kwa mtu. Adui wa Mdude ni mtu mmoja tu! Ni mtu asiyependa kukosolewa,” alisema Mwabukusi.

“Tunaitisha kwa upendo kuwasihi wahakikishe anapatikana salama, hilo ndio ombi letu vinginevyo tutaenda kuitisha a strong language (lugha kali) ambayo haijapata kutokea kabla,” alisema Mwabukusi.

Hivi karibuni Makamu Mwenyekiti wa Chadema, John Heche, aliandika katika ukurasa wake kwamba naibu katibu mkuu wa chama hicho, Amani Golugwa, atakwenda mkoani Mbeya kufuatilia suala la kupotea kwa Mdude.



Rais
wa TLS,
Boniface
Mwabukusi



Uchumi & Biashara

Bandari kuziweka karibu Tanzania, DRC



Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile

Na Mwandishi WETU, Dodoma

SERIKALI ya Tanzania kwa kushirikiana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), zimesaini hati ya makubaliano yanayolenga kuboresha miundombinu ya usafirishaji, ikiwemo bandari.

Makubaliano hayo ni sehemu ya jitihada za pamoja za kukuza biashara ya mipakani, hususan kupitia Ziwa Tanganyika, ambapo Tanzania inaendelea na ujenzi wa Bandari ya Karema mkoani Katavi pamoja na maboresho ya Bandari ya Kigoma.

Akijibu swali la Mbunge wa Momba, Condester Michael Sichalwe, aliyetaka kujua hatua ambazo zinachukuliwa na serikali kuhakikisha Tanzania inanufaika na soko la DRC licha ya nchi hiyo kutoanza ujenzi wa bandari upande wake, Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Ki-

henzile, alisema serikali imejipanga kikamilifu kushirikiana na DRC kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Alisema serikali inaamini kuwa ushirikiano huo utafungua fursa za kiuchumi baina ya nchi hizo mbili kupitia sekta ya usafirishaji ikiwemo bandari.

“Serikali kupitia TPA imeanza uboreshaji wa Bandari ya Kigoma pamoja na ujenzi wa Bandari mpya ya Karema katika kwa lengo la kushirikiana na DRC katika kukuza biashara kupitia Ziwa Tanganyika,” alisema Kihenzile.

Naibu waziri huyo alieleza Bunge kuwa tayari TPA inaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili ya kuendeleza Bandari ya Moba upande wa DRC, huku ujenzi wa Bandari ya Karema ukiendelea kwa ushirikiano na mwekezaji binafsi.

Lakini, pamoja na mradi huo wa uendelezaji wa bandari, Mbunge Sichalwe aliitaka serikali kuchukua hatua zaidi kwa kuhakikisha kunakuwa na barabara ya moja kwa moja kutoka Bandari ya Moba hadi Lubumbashi nchini DRC, ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na kuepuka usumbufu wa kupitia Zambia.

“Mheshimiwa naibu waziri, ulipokutana na meneja wa TPA, alisisitiza umuhimu wa barabara ya Moba hadi Lubumbashi. Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha ujenzi wa barabara hiyo unaanza?” alihoji Sichalwe.

Akijibu hoja hiyo, Naibu Waziri Kihenzile alikiri kuwa barabara hiyo kuwa ya kimkakati na serikali imejipanga kuhakikisha kuwa miundombinu ya kuunganisha masoko ya DRC, hususan Lubumbashi, inaboreshwa.

Aliongeza kuwa Tanzania ina fursa ya kipekee ya kuhudumia nchi zisizo na bandari kama Zambia na DRC, ambapo kwa sasa Zambia hupitisha zaidi ya tani milioni saba za mizigo kupitia Tanzania, huku DRC ikifikia zaidi ya tani milioni 10.

“Tunaendelea kuwekeza katika bandari zetu za mikoa ya Ziwa Tanganyika ili kufungua fursa zaidi kwa wafanyabiashara wetu,” alisema naibu waziri huyo.

Leseni 95 za madini hatarini kufutwa

Na Mwandishi WETU

SERIKALI imetoa hadi Mei 13 mwaka huu kwa kampuni 95 kubwa na za kati za uchimbaji madini, kujieleza kwa nini leseni zao zisifutwe kutokana na kukiuka masharti.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, wakati alipokuwa anawasili-sha bajeti ya wizara hiyo bungeni jijini Dodoma.

Mavunde aliwaambia wabunge kuwa mmiliki wa leseni ambaye atashindwa kutoa maelezo ya kuridhisha hadi tarehe hiyo, basi leseni yake itafutwa na Tume ya Madini.

Onyo hilo limetokana na kampuni hizo kushindwa kuanza kuendeleza maeneo yao ndani ya kipindi cha miezi 18 inayotakiwa kisheria baada ya kupata leseni.

Waziri Mavunde alithibitisha kuwa wamiliki wa leseni hizo wanapaswa kutoa maelezo kwa nini wameshindwa kutekeleza masharti ya leseni zao ifikapo Mei 13, mwaka huu na iwapo watahindwa kufanya hivyo, basi leseni zao zitafutwa.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde

Kati ya leseni hizo ambazo hazijafanya kazi zipo za miradi saba ambayo uwekezaji wake unafikia shilingi trilioni 15.

Aidha, katika hotuba yake hiyo, Mavunde alisema kuwa kati ya Julai, mwaka jana na Machi mwaka huu, jumla ya leseni 8,501 za madini zilitolewa na Tume ya Madini katika lengo la kutoa leseni 10,294.

Pamoja na kutoa leseni, Mavunde alisema kuwa katika kipindi hicho serikali pia imefuta leseni 14 za wafanyabiashara ambao walikiuka masharti ya leseni zao.

Kati ya leseni zilizotolewa kulikuwa na leseni moja ya mradi maalum wa uchimbaji madini, leseni 25 za uchimbaji madini, leseni 396 za utafutaji madini, na leseni 6,227 za wachimbaji wadogo wadogo.

Mavunde pia aliliambia Bunge kuwa Tume ya Madini pia ilitoa leseni kwa mawakala 548 wa biashara ya madini, leseni 1,290 kwa madalali, leseni moja ya uchenjuaaji na leseni 13 za uchakataji wa madini.

Kati ya Julai 2024 na Machi 2025, jumla ya watafutaji wa madini 118 na wachimbaji wa kati 41 walipewa maonyo kutokana na kukiuka masharti ya leseni zao.

Wengi wao walishindwa kulipa ada za leseni za mwaka au kutoendeleza maeneo yao ya uchimbaji.

Kutokana na kushindwa kufanya marekebisho, serikali ilizifuta leseni tano za utafutaji wa madini na leseni tisa za uchimbaji kati ya zile zilizopewa onyo.

Waziri Mavunde pia alitangaza kuwa leseni za uchimbaji mdogo wa madini zimetolewa katika maeneo mapya 65 yenye madini ikiwemo Geita, Mara, Mbogwe, Kahama, Chunya na Songwe.

Aidha, sampuli 972 za makinikia kuto-
ka mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu, Katavi
Mining Company Limited, Jiuxing (TZ) Min-
ing Limited na ZEM (T) Company Limited zili-
fanyiwa majaribio, pamoja na sampuli 4,011 za
wateja binafsi waliotaka kupata taarifa za kina
kuhusiana na hali ya madini katika maeneo yao.

Makala Maalum

Tazara na hadithi ya kapu lililotoboka

USAFIRI wa Treni ya Tazara ulikuwa mkombozi na taa yenye mwanga wa neema kwa wananchi wa Tanzania, Zambia na hata China. Hata hivyo, matumaini yote yalizimwa baada ya safari za reli hiyo kusuasua na hatimaye kusimama kwa muda. Makala haya maalum yanaeleza adha ya kutofanya kazi vyema kwa usafiri huo.

Picha zote na Simon MKINA

Makala Maalum

Tazara na hadithi ya kapu lililotoboka

Na Simon MKINA, Lusaka

MIALE ya jua la utosi inachoma wanaotembea maeneo ya Jiji la Dar es Salaam, lakini wengi hawajali – kila mmoja anaendelea na shughuli zake.

Ni majira ya saa 7:00 mchana, ambapo abiria wanaosafiri kwa basi la ABC, wamekusanyika eneo la Manzese, zinakopatikana ofisi za basi hilo.

Abiria wanapanda kuingia ndani ya basi hilo tayari kwa safari ya kilomita 925 kuelekea Tunduma, mji wa mpakani eneo la Tanzania, unaopakana na Mji wa Nakonde, ulioko Zambia.

Baada ya abiria kuingia ndani ya basi na kukeki, safari ndefu ya saa 18 inanza, huku dereva akiendesha kwa umakini kukwepa vurugu za wapita njia, baiskeli, pikipiki na hata magari mengine “yenye haraka.”



Abiria wakiwa ndani wa treni ya Tazara

Manzese ni miongoni mwa maeneo yenye pilikapilika na vurugu nyingi katika Jiji la Dar es Salaam.

Safari inaendelea na basi linaacha “vurugu za barabara za Dar es Salaam, linaingia Mkoa wa Morogoro na njiani kuna magari makubwa ya mizigo.

Haya yanakwenda kwa mwendo mdogo. Hayana kasi sana kwa kuwa yamebeba mizigo inayopelekwa nje ya mipaka ya Tanzania, na hasa Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Zimbabwe.

Msululu wa magari haya ya mizigo, ni matokeo ya kukosekana kwa usafiri wa uhakika na nafuu zaidi; Treni ya Tazara, baada ya safari zake kutoka Dar es Salaam hadi Nakonde, Zambia kusimamishwa.

Basi “linachanja mbuga” na kuingia Mkoa wa Iringa, ambapo barabara finyu, kuelekea Tunduma, pia inafanya mwendo wa basi kuwa mdogo, hivyo kuongeza muda wa kuwa njiani. Hakuna njia mbadala.

Mwendo wa basi unakuwa mdogo zaidi – kama kusindikiza maharusi, baada ya kufika maeneo yenye milima, hasa Kitonga, kwani idadi ya malori inaongezeka.

Alfajiri ya siku inayofuata – wakati basi likielekea Tunduma, abiria ndani ya basi wanaashuhudia idadi kubwa zaidi ya malori pembezoni mwa barabara, mengine yakiwa yamepaki kwenye maeneo ya wazi na baadhi yakiwa yanaendelea kusafiri.

Yote haya yanaelekea nje ya mipaka ya Tanzania. Malori hatari pamoja kwamba sehemu kubwa ya barabara za Tanzania kuwa nzuri, lakini yapo maeneo, kwenye Barabara ya Dar es Salaam – Tunduma, yameharibika. Waharibifu hawa ni malori.

Gazeti la Pambazuko limeshuhudia maeneo kadhaa ya barabara za Mkoa wa Songwe, ambayo “hailali” kwa wingi wa safari za malori ya mizigo, zikiwa mbovu.

Mmoja wa abiria ndani ya basi, Mussa Kiwanga, mfanyabiashara wa vifaa vya nyumbani, anayebeba bidhaa kutoka Dar es Salaam kupeleka Ndola, Zambia, anasema ongezeko la malori, ndiyo chanzo kikubwa cha kuharibika kwa Barabara ya Tunduma.

Inaendelea Uk. 22

Makala Maalum

Tazara na hadithi ya kapu lililotoboka

Inatoka Uk. 21

“Malori yamekuwa yakiharibu sana barabara, tena yanaendelea kuwa mengi baada ya usafiri wa Treni ya Tazara kusimama,” anasema Mussa.

Mussa anasema kuwa wakati Treni ya Tazara ikifanya kazi, idadi ya malori haikuwa kubwa kama inavyoshuhudiwa sasa.

Kama inavyoelezwa na wafanyabiasha wengi wanaotumia malori kusafirisha mizigo yao sasa, Mussa analaumu kusimamishwa kwa usafiri huo, huku akieleza masikitiko yake kutumia gharama kubwa kusafirisha bidhaa tofauti na hali ilivyokuwa wakati akitumia usafiri wa treni.

Pamoja na kufika salama Tunduma, abiria wengi walisikika kulalamika uchovu wa safari ndefu. Baada ya basi kusimama, kituo cha mwisho – eneo jirani na mageri yanayotenganisha mpaka wa Tanzania na Zambia, abiria wengi walishindwa kuvaa viatu kutokana na miguu kuvimba.

Baada ya kufika Tunduma, Pambazuko lili fuata taratibu za kuvuka mpaka kutoka Tanzania kuingia ardhi ya Zambia, ikiwamo kupata visa ya kuingia nchi hiyo.

Ofisa Uhamiaji wa Tanzania alichukua pasipoti na kugonga mhuri wa kutoka na baadaye Pambazuko kuelekezwa kwenda kaunta ya Ofisi za Uhamiaji Zambia.

Hapo Ofisa wa Uhamiaji Zambia alipokea pasipoti na kuulizwa maswali kadhaa ikiwamo sababu za kuingia nchini mwao.

Hata hivyo, jibu moja lilikuwa gumu baada ya kuhojiwa kuhusu cheti cha chanjo dhidi ya homa ya manjano. Pambazuko halikuwa na cheti hicho. Pamoja na kuomba ili kuruhusiwa kuingia Zambia, ofisa huyo alikataa.

Ofisa huyo hakutaka kusikiliza lolote, ndipo baadaye akaomba rushwa – bila woga kwamba



Chumba cha abiria maarufu (VIP) kusibiri treni katika stesheni ya New Kapiri Mposhi, Zambia

anataka shilingi 50,000 za Tanzania ili kugonga visa na kupewa cheti hicho.

Pambazuko “lilitoa rushwa” hiyo na kuruhusiwa kuendelea kuvuka mpaka.

Lengo la Pambazuko lilikuwa kupanda Treni ya Tazara – ambayo kwa upande wa Zambia bado inafanya safari zake kutoka Nakonde hadi New Kapiri-Mposhi, hata hivyo usafiri huo haukuwepo siku hiyo, baada ya kuelezwa kuwa unapatikana siku mbili tu kwa wiki; Jumanne na Ijumaa.

Hivyo, usafiri wa basi ndiyo ikawa njia muhimu ya kufika Lusaka, Mji Mkuu wa Zambia.

Ndani ya basi la Royal, safari kilomita 1,020 - inayotumia saa 17, ilianza mchana saa 8:30, kutoka Nakonde hadi Lusaka. Tiketi ya basi iliandikwa safari ingeanza saa 6:00 mchana.

Safari iliendelea vyema na ilipotimu saa 5:40 usiku, abiria walielezwa kuwa kutakuwa na mapumziko na kupata chakula katika mji wa Serenje, ambapo basi lingeendelea kwa safari kuelekea Lusaka saa 10:00 alfajiri.

Miguu ya kuku

Baada ya kufika Serenje, abiria walishuka na kuelekea kwenye migahawa kwa ajili ya kupata chakula, huku wengine wakielekea kwenye baa za jirani kwa kupata vinywaji.

Wazambia wengi – hasa waliokuwamo ndani ya baa, walionekana kuwa wakarimu kwa wageni.

Inaendelea Uk. 23

Makala Maalum

Tazara na hadithi...



Abiria wakiwa ndani ya treni ya Tazara

Inatoka Uk. 22

Abiria walioingia kwenye moja ya migahawa hiyo, ikiitwa Kapele, waliagiza vinywaji, na punde wahudumu walipitisha miguu ya kuku iliyochemshwa, wakieleza kuwa hiyo ni “appetizer” kwa wateja wao.

Miguu ya kuku ni maarufu kwa jina la “impompo” kwa Kabila la Chichewa.

Pambazuko lilionja na kubaini kuwa miguu hiyo inachemswa kwa kuwekwa chumvi, vitunguu na tangawizi.

Kila mteja aliruhusiwa kuchukua mguu

mmoja, huku ikielezwa kuwa anayependa kuongeza, atalazimika kununua kwa Kwacha 5 (sawa na Shilingi 500). Pambazuko liliongeza miguu miwili.

Katika baa hiyo, Pambazuko lilishuhudia kukosekana kwa kifungulio cha chupa yenye kinywaji (opener). Kwamba meno ya wahudumu ndiyo yalitumika kuwa mbadala.

Kila bia inaponunuliwa, mhudumu anaifungua kwa meno na pengine, akiwa na kiu, anakunywa fundo kabla ya kumpa mteja. Ukarimu wa Zambia huo!

Jambo jingine la kushangaza kwa Wazambia ni kwamba mnapokuwa baa, haijalishi mnajua na ama hamjuani, jirani yako anaweza kuchukua bia yako akanywa bila kuomba wala kuruhusiwa. Ni utamaduni wao.

Safari ya kurudi

Baada ya kukaa kwa siku mbili Lusaka, likihoji wafanyabiashara waliokuwa wakitumia Treni ya Tazara, Pambazuko lilianza safari kurejea Nakonde na baadaye Dar es Salaam.

Pambazuko lilitumia usafiri wa basi kutoka Lusaka hadi New Kapiri-Mposhi, ambako lilipanda Treni ya Tazara kuelekea Nakonde.

Treni hiyo iliyokuwa iondoke saa 6:00 mchana, ilianza safari baada ya saa mbili. Hakuna maelezo yoyote yaliyotolewa na uongozi kwa kuchelewa.

Ikiwa ni umbali wa kilomita 818 na kutarajiwa kutumia saa 12, lakini ilichukua saa 16 kufika Nakonde, baada ya treni kuharibika katika eneo la Chozi.

Ndani ya mabehewa, hasa yale ya daraja la pili na tatu, abiria walikuwa wengi kupita kiasi, wengine wakikaa njia za kupita, wengine wakawa wameketi ama kusimama maeneo ya vyoo.

Ndani ya vyoo hakuna maji, achilia mbali karatasi za kujiweka safi baada ya haja.

Ndani ya mabehewa hayo, watoto wanalia kutokana na msogamano wa watu na kupungua kwa hewa, huku harufu nzito na mbaya zikihihiwa kutokana na vyakula vilivyobebwa, mifugo; kuku na bata ambao wanaonekana wamefungwa kamba na kuhifadhiwa chini ya viti.

Hakika hakuna raha kusafiri na Treni ya Tazara katika mazingira ya sasa. Ni kero!

Inaendelea Uk. 25

Mtoto wa Mvuvi

Na Maregesi PAUL

Watu wasiojulikana wanaishi wapi?



WANANCHI wanalamika kila mahali kuhusu usalama wa nchi yetu.

Hawalalamiki kwa sababu wana-taka kulalamika, bali wanalamika kwa saba-bu kuna watu wasiojulikana ambao wamekuwa wakifanya uhalifu katika maeneo mbalimbali nchini bila kukamatwa kwa sababu hawaju-likani.

Viongozi wenye dhamana ya kuwalinda wa-nanchi wanalamika ingawa wana silaha na vi-tendea kazi vingi vya kukabiliana na wahalifu.

Viongozi wa dini wenye kibali cha kukemea na kuwaomba wananchi wote wakiwamo watu wasiojulikana, wanalamika.

Vyombo vya ulinzi na usalama navyo vinalalamika ingawa havitoi sauti.

Hakika hali siyo shwari ndiyo maana malala-miko ni mengi kuhusu usalama wa wananchi unaotikiswa na watu wasiojulikana.

Inaonekana watu wasiojulikana wana mbinu zaidi ya vyombo vyetu vya ulinzi, inaonekana watu hao wana maarifa mengi, ujasiri, mbinu, mikakati na upeo mpana wa kuvikwepa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama.

Hawa watu wasiojulikana wanaweza kum-shusha abiria kwenye basi mchana kweupe na

kwenda kumuua, watu wasiojulikana wanaweza kumvamia kiongozi wa dini na kumjeruhi vi-baya akiwa katika makazi yake.

Yaani, watu wasiojulikana wanaweza kuteka, kuumiza mtu au watu na kuwapeleka kusikojuli-kana bila kujulikana kwa sababu hawajulikani.

Kwa hakika, hali ni mbaya sana, hofu ni kub-wa mno, manung'uniko ni mengi nchini kwa sababu hadi sasa hajapatikana mtu aliyeweza kusimama na kuwaambia Watanzania, kwamba watu hao wasiojulikana wanaishi wapi.

Hakuna anayeweza umma kama watu hao wasiojulikana wanakutana katika maeneo gani kwa ajili ya kupanga uhalifu wao.

Kwa hiyo, umefika wakati sasa tushikamane kuwauliza wenye mamlaka ya kuwalinda wana-nchi watuambie watu wasiojulikana wanaishi wapi?

Watuambie watu hao ni kabila gani na wasi-ogope kutuambia watu hao wanaokatisha hata uhai wa watu wakoje.

Ni vyema sasa vyombo vya ulinzi na usala-ma viwaambie Watanzania nini kifanyike kuji-linda dhidi ya watu hao.

Watu hawa wasiojulikana wameweka maisha ya watu kwenye wasiwasi mkubwa kila uchao. Hakuna mwenye uhakika wa kuona dakika chache zinazofuata, kwani anaweza kupotezwa. Hakuna mwenye amani.

Ninasema hivyo kwa sababu huku mtaani tunakoishi hali ni tete. Wananchi wanalamika sana, waumini makanisani na misikitini wana-pishana kuliomba taifa ingawa baadhi wanase-ma ovyo dhidi ya serikali yao.

Kwamba serikali ndiyo yenye dhamana ya kuwalinda, iweje ikae kimya?

Kila Mtanzania anatamani kuona serikali yake ikiwajibika kuwadhibiti watu wasiojuli-ka-na ambao wanasabisha waishi bila kujua usala-ma wa leo na kesho yao.

Kwa kuwa lengo langu kwa niaba ya Wataza-nia ni jema, bado ninazidi kusema na kuuliza, hao watu wasiojulikana wanaishi wapi ili tuwa-jue na kuwaomba kwa Mwenyezi Mungu ili awabadilishe na kuwafanya watu wema.

Makala Maalum

Tazara na hadithi...



Biashara ya fedha katika mpaka wa Zambia na Tanzania eneo la Nakonde.

Wafanyabiashara walia

Watu 32 – wengi wakiwa wafanyabiashara waliokuwa wakifurahia usafiri wa Treni ya Tazara, wamezungumza na Pambazuko na kudhihirisha namna kusimamishwa kwa usafiri huo wa treni ulivyoharibu mfumo wa maisha “mazuri” waliyozoea kwa kutumia Tazara kusafrisha biashara zao kutoka ama kwenda Tanzania - Zambia na nyingine jirani.

Wanaomba usafiri huo urejeshwe haraka, na ikiwezekana uwe umeboreshwa ili kuwaongezea faida kwa biashara zao, badaya ya kuendelea kutumia usafiri wa barabara ambao wamesema ni aghali zaidi.

Sababu za kusimama treni

Ofisa Mwandamizi wa Huduma za Wasafiri wa Tazara, kwa upande wa Tanzania, Benson Magoha, ameliamba Pambazuko kwamba usafiri wa treni hiyo kutoka Dar es Salaam hadi New Kapiri-Mposhi ulisimamishwa tangu Juni 18, 2024.

Huku akiwa mwangalifu kwa matamshi yake, bila kuingia kwa undani sababu za kusimamishwa kwa usafiri huo, Benson amesema; “shida ni vifaa, injini zimekuwa za muda mrefu, sasa kuna vitu vinafanyika, na karibuni safari zaitaanza.”

Tazara kapu la hasara

Ilikuwa furaha, vifijo na shangwe kwa wananchi wa mataifa mawili jirani; Tanzania na Zambia waliposhuhudia kuzinduliwa kwa usafiri wa treni kutoka Dar es Salaam hadi Kapiri-Mposhi.

Furaha ya wananchi hao ilibebwa na kuwepo kwa uhakika wa safari zao kutoka sehemu moja hadi nyingine – kwa pengine gharama nafuu.

Hata hivyo, mbali na furaha kwa wananchi wa Tanzania na Zambia, pia kulikuwa na nchi nyingine, ambayo siyo jirani; China, ambayo iligundua kuwepo kwa faida kubwa ya kiuchumi kuzitumia nchi hizo mbili za Afrika, kusafrisha malighafi kutoka Zambia, kupitia Tanzania, hadi nchini kwake.

China iliona fursa kubwa ya kusafrisha shaba kutoka Zambia hadi kwake – umbali unaokadiriwa kuwa kilomita 13,500 kwa usafiri wa ardhini, kwa ajili ya matumizi ya viwanda, ambavyo wakati huo vilikuwa vimeanza kuenea.

Katika kukamilisha ndoto yake ya kupata shaba kwa wingi, China ilikubaliana na Tanzania na Zambia kutoa mkopo usiokuwa na riba kwa nchi hizo ili kutandaza reli yenye urefu wa kilomita 1,860 - kwa ajili ya usafiri wa treni kutoka Kapiri-Mposhi hadi Dar es Salaam, ambapo shaba ingepakiwa kwenye meli na kusafrishwa hadi China.

China ilitoa dola za Marekani milioni 412 (zaidi ya Shilingi trilion moja) na ujenzi kumilika mwishoni mwa mwaka 1975 -na kuanza kazi rasmi Julai 14, 1976.

Reli hiyo yenye madaraja 274, huku ikipita kwenye mahandaki (tunnels) 19 ilipewa jina la Tazara; ikiwa ni kifupi cha Tanzania and Zambia Railway Authority. Pia ina jina lingine la “Reli ya Uhuru.”

Mikopo isiyoleta matunda

Mradi wa Reli ya Tazara unaweza kuwa moja ya “kapu lililotoboka” ambalo limeshindwa kujaa kutokana na fedha nyingi za mikopo nafuu kutoka China kushindwa kuleta matokeo chanya.

Ukiacha mkopo mkubwa – usiokuwa na riba wa kuanza ujenzi wa reli hiyo uliotolewa hadi mwaka 1975, China ililazimika kuongeza mikopo mingine zaidi, baada ya miaka 25 tangu kuanza kazi kwa Tazara. **Inaendelea Uk. 26**

Makala Maalum

Tazara na hadithi ya kapu lililotoboka

Inatoka Uk. 25

Tovuti inayoratibu mlolongo wa mikopo na misaada kutoka China, inaeleza kuwa kwa kipindi cha miaka 13, kuanzia mwaka 2001 hadi 2014, nchi hiyo imetoa kiasi cha dola za Marekani milioni 109.77 kuhuisha Reli ya Tazara.

Mbali na fedha hizo, pia vyanzo vingine vinaonyesha kuwa Machi 26, 2012, China iliipatia Tazara dola milioni 66.2 zilitolewa na China ikiwa ni mkopo nafuu kwa ajili ya matengenezo ya injini za treni ya Tazara, sambamba na kurekebisha baadhi ya mabehewa yaliyokuwa yameharibika.

Kama hiyo haitoshi, Julai 15, 2014, dola za Marekani 80 milioni, zilitolewa na serikali za Tanzania na Zambia kuipa Tazara kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya mishahara, posho za wafanyakazi na kiasi kingine kwa ajili ya shughuli za utawala.

Pamoja na fedha hizo, na zikijumuishwa na zingine ambazo Tazara ilikuwa ikipokea kutokana na mauzo ya tiketi na mizigo, bado mradi huo umeshindwa kujiendesha na kuleta faida kwa Tanzania na Zambia, achilia mbali kutoa gawio la faida kwa nchi hizo mbili.

Sasa China kuisimamia

Kutokana na Tazara kushindwa kutengeneza faida na hata kujiendesha – ikiwa inakadiriwa kubeba abiria wanaofikia milioni 60 tangu kuanzishwa kwake, hatimaye mkataba kati ya

China kupitia kampuni yake ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) inawekeza dola za Marekani bilioni 1.4 kuiendesha kwa miaka 30.

Mkurugenzi Mtendaji wa Reli ya Tazara, Bruno Ching'adu amesema uwekezaji kutoka CCECC haurekebisha tu miundombinu ya reli, bali pia utafanya reli kuwa mwezeshaji muhimu wa biashara na ukuaji wa uchumi kati ya Tanzania na Zambia.

Fedha hizo zitatumika kununua vichwa 32 vya treni, pamoja na mabehewa ya mizigo 762.

Katika miaka 30 ya uendeshaji; miaka mitatu ya mwanzo itatumika kufanya matengenezo na miaka 27 itatumika kuendesha reli hiyo.

Hii maana yake ni kwamba Wachina ndiyo watakuja kusimamia kila kitu kuanzia matengenezo, ununuzi, mapato na matumizi kwa kipindi cha miaka hiyo 30.

Haya ni matokeo ya kushindwa kuendesha reli hiyo iliyokuwa inabeba matumaini ya wananchi katika kukuza uchumi, lakini haikuwa hivyo, isipokuwa kuandika “maumivu ya hasara” tangu kuanzishwa kwake miaka 50 (nusu karne) iliyopita.

Makala haya yanayoangazia hali ya usafiri maeneo ya mipaka ya Afrika ‘Borderlands,’ ni mfululizo mpya kwenye gazeti la The Continent. Mfululizo huu umewezeshwa na Umoja wa Afrika (AU) na GIZ. Imeandikwa na Pambazuko

Na Rashid
MTAGALUKA



Hoja Yangu

Mazonge matumizi fedha za mfuko wa jimbo

MALALAMIKO ya Mbunge wa Jang'ombe, Ali Haasan 'King,' kuhusu ukosefu wa usawa katika mgawanyo wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, aliyoyotoa bungeni karibuni, yanaibua hoja pana zaidi.

Kwamba je, wananchi wa majimbo yote wanajulishwa na kuelewa matumizi ya fedha hizi? Au mijadala ya wabunge inabaki kuwa ya malalamiko ya nyongeza bila ushirikishwaji wa waliowatuma bungeni?

Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi mdogo ya maendeleo inayogusa maisha ya wananchi moja kwa moja.

Fedha hizi hutolewa kila mwaka kwa kila jimbo na kusimamiwa na mbunge kwa kushirikiana na kamati ya maendeleo ya jimbo.

Kisheria, matumizi yake yanapaswa kuakisi mahitaji ya wananchi, hivyo inapaswa kuandaliwa vikao vya hadhara kujadili mipango ya matumizi.

Hata hivyo, hali halisi inadhihirisha pengo kubwa katika ushirikishwaji wa wananchi. Katika maeneo mengi, wananchi hawaelewi kiasi cha fedha kinachopokelewa, miradi iliyopangwa, wala namna ya utekelezaji.

Hii inaleta shaka kuhusu uwazi na uwajibikaji wa wabunge na kamati husika. Wananchi hujikuta wakishangaa kuona ujenzi wa daraja, kisima, au ukarabati wa shule ukiitwa "mradi wa jimbo" bila kufahamu fedha zilitoka wapi, zilitarajiwa kutumika kiasi gani, na kwa muda gani.

Ni kweli kwamba baadhi ya wabunge hufanya juhudi za kuitisha mikutano ya hadhara, kutoa taarifa za maendeleo, na kuomba maoni ya wananchi kabla ya matumizi ya fedha hizo.

Lakini kwa kiasi kikubwa, vikao hivyo havijawekwa kama utaratibu wa lazima, hivyo baadhi ya wabunge huona siyo lazima kuvitisha.

Badala yake, mijadala mingi hujikita katika kulalamikia kiwango kidogo cha fedha au tofauti ya mgao bila kuangalia namna bora ya kusimamia kilichopo.

Kwa upande wa Zanzibar, hoja ya King inagusa kiini cha mjadala wa usawa na kimuundo kati ya sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano.

Ikiwa kweli majimbo ya Zanzibar hupokea mgao mdogo kulinganishwa na yale ya Bara, ni muhimu hoja hiyo ijadiliwe kiseri na kwa takwimu.

Hata hivyo, bila kujali kiwango, hoja ya msingi ni kuhakikisha wananchi wanajua, wanaelewa, na wanashiriki katika ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za mfuko wa jimbo.

Kwa ujumla, kuna haja ya kuimarisha mifumo ya uwazi na uwajibikaji kwa wabunge wote kwa kuweka utaratibu wa lazima wa mikutano ya kutoa taarifa kwa wananchi kila mwaka.

Pia elimu kwa umma kuhusu mfuko huu inapaswa kupewa kipaumbele, ili kuondoa hali ya fedha kutumika kana kwamba ni mali ya mtu binafsi, badala ya kuwa chombo cha pamoja cha maendeleo.

Mwandishi anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Mbunge wa Jang'ombe, Ali Haasan 'King,'

Riwaya

Viaticum-33

Sakramenti ya Mwisho



Kwa wasomaji wapya: Eddy anapatwa mawazo mengi kufuatia kifo cha ghafla cha Masenya, lakini anachanganyikiwa zaidi kutokea kwa kifo kingine. Je, ni kifo cha nani? Endelea kufuatilia riwaya hii ya tamu ya kijajusi...

Na Godwin Chilewa, Houston, MAREKANI

“TATIZO ni ubovu wa barabara zetu,” mwingine alidakia kwa hasira.

“Hapana, tatizo siyo barabara, bali utaratibu mbovu wa utoaji leseni. Siku hizi watu hawafanyi driving test, wanahonga tu, halafu leseni wanapelekewa nyumbani.

“Kweli kabisa,” mwingine alidakia.

“Sweden mtu hapewi leseni mpaka amefundishwa na kufuzu kwelikweli. Kule ni rahisi kupata degree kuliko leseni ya kuendesha gari...”

“Itachukua miaka kumi na tano mingine kusomesha mtu wa kuziba pengo la Dokta Mushi,” dada mmoja alidakia kwa uchungu.

Ili mradi kila mtu alizungumza lake, na kwa uchungu kuhusu vifo vya watu hao na wengine

wengi waliopoteza maisha yao kwa ajali.

Kwa Eddy asiyemfahamu Dokta Mushi, maneno hayo yalimfanya akumbuke mauaji ya rafiki na bosi wake wa zamani, inspekta Hatibu, ambaye pia alikuwa hazina kubwa kwa Taifa.

Akaenda mbali zaidi kuwakumbuka marehemu Mbaraka Mwishehe, Masia Radi na Mtooto wa Dandu, hawa ni wanamuziki maarufu wa nyakati tofauti tofauti waliopoteza maisha yao kwa ajali za magari.

Mjadala huo uliendelea kwa nusu saa hivi. Baadaye watu wakaacha kuzungumzia ajali wakaingia kwenye kujadili ongezeko la matukio ya uhalifu kasha wakaendelea na michezo yao.

Eddy pia mawazo yake yakarudi kwenye kifo cha Masenya. Akakumbuka jinsi alivyomuona kwa mara ya kwanza pale kwenye chumba cha kuhifadhi maiti, Hospitali ya Bugando.

Akakumbuka jinsi alivyokuwa muungwana kiasi cha kukubali kumpa nakala kivuli ya cheti cha kifo cha askofu Lucas Simba; na jinsi alivyokuwa tayari kumpa taarifa nyingine za zia-da ambazo mpaka wakati huo hakujua zilihusu jambo gani.

Wakati akitafakari hayo, akahisi mapigo ya moyo wake yakiongezeka kama mtu aliyeona kitu cha hatari.

“Askofu Simba ni mtu mkubwa sana. Hapa mjini Mwanza anajulikana kuliko hata Mkuu wa Mkoa, kwa hiyo naamini uchunguzi wa kifo chake utafanywa na Dokta Evance Mushi...”

“Yeye ndiye daktari bingwa pekee wa uchunguzi wa maiti (pathologist) katika kanda ya ziwa,” haya yalikuwa maneno ya Masenya aliyomwambia Eddy kwenye chumba cha maiti hospitalini Bugando.

Muda huu maneno hayo yalijirudia kichwani mwake kama wimbo uliorekodiwa kwenye CD.

“Pengine siyo yeye aliyefanya uchunguzi huo,” alijisemea kwa kujifariji.

Lakini kabla wazo hilo halijaota mizizi kichwani mwake, akakumbuka nyaraka alizopewa na Mwaluko kule hospitalini baada ya kupelelelelwa maagizo na Masenya.

Karatasi iliyoeleza sababu za kifo cha Askofu Simba iliandikwa jina la daktari Evance Mushi (Pathologist) na kutiwa saini kwa mkono wake.

Inaendelea Uk. 29

Viaticum-33

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

Huu ulikuwa ushahidi usio shaka kwamba yeye ndiye aliyefanya uchunguzi wa kifo cha Askofu Simba.

Kwa kifupi watu wawili waliohusika na uchunguzi wa kifo cha Askofu Lucas Simba walikuwa wamepoteza maisha yao saa chache tu baada ya kukamilisha uchunguzi na kutoa ripoti.

“Kwanini? Hili ni jambo la nasibu tu au ni kitu kilichopangwa? Eddy alijiuliza huku nywele zikimsisimka.

Hakuwa na shaka kwamba kifo cha Masenya kilipangwa, maana aliuawa kwa kuchinjwa. Lakini je, vifo vya Dokta Mushi na mkewe navyo vilipangwa au vilitokana na ajali ya gari tu?

Kama vifo vya watu hawa ni vya kawaida, basi hakuna shida, lakini kama vifo vyao navyo vilipangwa kama kifo cha Masenya, basi kuna kitu kisicho cha kawaida. Alifikiria mno kuhusu matukio haya.

“Vipi kama vifo vya Dokta Mushi na mkewe vina uhusiano na kifo cha Masenya, lakini havi-na uhusiano wowote na kifo cha Askofu Simba?” Alijiuliza.

“Dokta Mushi na Masenya wote wameuawa katika mazingira korofi, lakini Baba Askofu amekufa akiwa usingizini, kwenye jumba la watakatifu. Inawezekanaje kifo chake kiwekwe kundi moja na akina Masenya? Alitafakari.

Wazo hilo lilipingwa vikali na ukweli kwamba Masenya alitaka kumueleza jambo fulani muhimu baada ya kumpatia nakala ya uchunguzi wa kifo cha Askofu Lucas Simba. “Kwa vyovyote, kuna kitu kinachohusiana,” Eddy alihitimisha mawazo yake. Na sasa swali la msingi likamjia tena kichwani. “Nani aliyemualika kuhudhuria misa ya watakatifu? Kwa nini alimualika?”

Kufuatia mlolongo wa maswali haya akaona ipo haja ya kuendelea kuwepo mjini Mwanza kwa siku nyingi zaidi.

Alijiona ana wajibu wa kufuatilia kwa kina sababu za kifo cha Masenya. Alikuwa na haki-

ka kama akijua sababu zilizofanya au awe, bila shaka atajua jambo alilotaka kumwambia, na kama kifo cha Askofu Lucas Simba kina uhusiano wowote na mauaji hayo.

Sambamba na hilo, aliona umuhimu wa kufuatilia kifo cha Dokta Evance Mushi ili aweze kujiridhisha kama ajali hiyo ilikuwa ya kawaida au ilipangwa kwa sababu yoyote ile.

“Kaka, nikuongeze kahawa nyingine au ungependa nikuletee kinywaji gani? Sauti ya mhudumu ilimshitua kutoka lindi la mawazo.

“Ahsante dada yangu, nipe kikombe kingine cha kahawa, na chupa kubwa ya maji ya kunywa,” alimjibu huku akijitahidi kutabasamu.

Mhudumu akanyanyua sinia la kukusanya vyombo akaondoka navyo kuelekea jikoni. Hazikupita hata dakika tatu akarudi akiwa ameshika kikombe kingine, kibirika cha maji ya moto na chupa ya maji ya kunywa.

“Ahsante sana,” Eddy alimwambia huku akipokea kikombe hicho. Akajitengenezea kahawa nyingine, akainywa haraka haraka.

Alipomaliza akamlipa mhudumu stahiki yake, akanyanyua chupa ya maji ya kunywa, akaondoka kwenda chumbani kwake. Ilikuwa imeshatimia saa tano kasoro robo usiku.

Itaendelea...



Barua za wasomaji**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz

Waziri Aweso tunakupongeza, lakini tatua hili

Mhariri,

NIMEMSIKILIZA Waziri wa Maji, Jumaa Aweso wakati akiwasilisha bajeti ya wizara yake, huku akielezea mafanikio mengi ya usambazaji wa maji nchini.

Tunampongeza kwa jitihada zake kuhakikisha wananchi wanapata maji.

Pamoja na hayo, kwa upande wetu sisi wakazi wa Mbezi kwa Musuguri eneo la Masaki, Dar es Salaam, tuna zaidi ya wiki mbili bila maji. Hii changamoto tumekaa nayo kwa muda mrefu sasa.

Kila tukiwasiliana na wahusika wa Dawa-sa- Kinyerezi, tunaambiwa maji ni ya mgao, hivyo tusubiri tutakuwa tukipata kila Alhamisi, lakini ahadi hiyo haijatekelezwa hadi sasa.

Tunakuomba mheshimiwa Aweso, tukumbuke sisi wakazi wa Mbezi-Masaki, tupate maji kama maeneo mengine maana tunateseka.

Jonathan Frank,

Mkazi wa Mbezi-Musuguri,

Barabara mbovu hadi lini?

Mhariri,

KWA mtu ambaye hafahamu vizuri Diji la Dar es Salaam akitokea mkoani na kupitia Barabara ya Morogoro, atahisi hakuna kero ya barabara katika jiji hili.

Nasema hivyo kwa sababu mtu huyo mgeni, atapokewa na barabara za kuvutia zenye mada-raja ya juu yanayopita magari na ya waendao kwa miguu.

Lakini ajabu ni kwamba atakapoanza kuingia mitaani, atashangazwa na namna barabara nyin-gi zilivyo mbovu kipindi hiki cha mvua na nyingi zikiwa zimejaa maji katika mahandaki na kute-ngeza madimbwi, huku zingine zikishindwa kupitika kabisa.

Kinachochocha na kukatisha tamaa zaidi, ni ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa kila mwaka na viongozi kuwa zitajengwa, huku wananchi wakiendelea kuteseka.

Mariam Joseph,

Mkazi wa Mbezi-Makabe

NUKUU *KUTEMBEA maeneo mapya na kukutana na watu wapya, ni darasa zaidi ya kuta nne za jengo la shule na walimu – Msemo wa Kijapani.*

Maoni ya Jaji Warioba yasipuuzwe

Mhariri,

HIVI karibuni Jaji Joseph Sinde Warioba alia-likwa kwenye mkutano wa Chama cha Wana-sheria Tanganyika (TLS) ambako alikuwa mi-ongoni mwa watoa mada.

Jaji Warioba alieleza namna yeye na Joseph Butiku - mara kadhaa walivyojaribu kuzu-ngumza na viongozi wa Chadema, akiwemo mwenyekiti wake, Tundu Lissu na makamu,

John Heche kuhusu umuhimu wa kurejea kwenye mazungumzo na viongozi wa CCM.

Serikali na Chadema ni vyema wakazingatia ushauri huo wa Jaji Warioba.

Kuanza upya wala siyo ujinga, maridhiano yarejeshwe kwa mustakabali wa nchi yetu.

Ally Rashid,

Sakina, Moshi, Kilimanjaro.



Kilimo-Hifadhi mkombozi wa wakulima

Na Mhandisi Isaria MWENDE

TANGU enzi, mwanadamu analima katika juhudi yake ya kujipatia chakula. Zana mbalimbali zime-tumika katika kilimo, ikiwemo za mkono, zin-azokokotwa na wanyama na hata zinazoendeshwa kwa mashine.

Zana hizi zilianza kwa kutengenezwa kwa miti na mawe hadi mwanadamu alipogundua chuma.

Baada ya mapinduzi ya viwanda, watu wengi walijiririwa kuzalisha viwandani na hivyo kuhitaji-ka kuondokana na kilimo cha kujikimu na kwenda kwenye kilimo cha kibiashara.

Mapinduzi ya viwanda yameleta maendeleo makubwa katika kilimo na kuwezesha matumizi ya zana ambazo zimepunguza harubu katika kili-mo, kuongeza uzalishaji kwa kuongeza maeneo ya kulima, kuweka mazingira rafiki zaidi ya uzalishaji na kuongeza ufanisi.

Matumizi ya zana katika kilimo ndiyo uti wa mgongo wa kilimo kwa maana bila matumizi ya zana, hakuna uzalishaji wenye tija. Hata hivyo, ma-fanikiao haya yameambatana na madhara.

Matumizi ya jembe la sahani linalokokotwa na maksai au linalofungwa kwenye trekta, limesababi-sha madhara kwenye udongo kwa sababu hufanya udongo kuwa laini na kuwa vumbi, hivyo hupepe-rushwa na upepo kwa urahisi kutoka shambani na kusababisha udongo kupoteza rutuba.

Eneo linapolimwa kwa jembe la sahani, ni sentimita 20 tu za juu za udongo zinazovurugwa.

Linapolimwa mfululizo, kusababisha tabaka gumu chini (hard pan) au jasi.

Uwepo wa hii jasi hufanya maji ya mvua kush-indwa kupenya na hivyo kusababisha yatiririke juu ya udongo na matokeo yake ni mmomonyoko wa ardhi ambao husababisha makorongo kwenye mashamba, kupotea kwa rutuba, viumbe hai na unyevunyevu.

Uwepo wa jasi pia huzuia hewa kupita, hu-fanya mizizi ya mimea kushindwa kupenya na hivyo kusambaa kwenye kina cha sentimita 20 tu. Maji kwenye udongo hupotea kirahisi kwa njia ya mvuke.

Ukiwepo ukame wa muda mfupi, mazao hunyauka kwa kukosa maji. Kwa ujumla, matumizi ya jembe la sahani husababisha kushuka kwa uzalishaji katika kilimo. Suluhisho la tatizo hili ni ku-tumia mbinu ya kulima maarufu kama Kilimo-Hi-fadhi. Kilimo-Hifadhi ni utaratibu wa uzalishaji katika kilimo unaozingatia matumizi ya mbinu sa-hihi za kilimo, zana sahihi zisizoharibu umbile la udongo na kuipatia mimea virutubisho, maji na hewa kwa mizania inayohitajika.

Kilimo-Hifadhi kinalenga kuwa na matumizi bora ya ardhi na kuendeleza hali ya asili ya udongo na hifadhi ya mazingira kwa ujumla.

Kilimo hiki huongeza na kuendeleza uwezo wa ardhi kutunza maji kwa muda mrefu, kuongeza virutubisho vya mimea, kuzuia mmomonyoko wa udongo na hatimaye kuongeza mavuno.

Inaendelea Uk. 31

Makala

Kilimo-Hifadhi...

Inatoka Uk. 31

Kilimo-Hifadhi kinatilia mkazo matumizi ya zana zinazopenya ardhini kwa kina kirefu zaidi kuliko jembe la mkono, plau ya kukokotwa na wanyamakazi na zile zinazokokotwa na trekta.

Zana hizi hupasua tabaka gumu la udongo (jasi) na hivyo kupunguza kasi ya maji ya mvua yanayotiririka juu ya ardhi, badala yake huingia ardhini na kuhifadhiwa kwa ajili ya mimea.

Endapo ukame wa muda mfupi utatokea, mazao hayaathiriki ikilinganishwa na eneo lililolimwa kwa plau.

Zana zinazopasua jasi hutumika katika kipindi cha mpito kutoka kilimo cha mazoea cha kutumia plau kwenda kwenye mbinu za Kilimo Hifadhi.

Mbinu ya pili ya Kilimo-Hifadhi ni kuacha mabaki ya mazao shambani, kuweka matandazwa (mulching) na kupanda mazao funika ili kuongeza mboji kwenye udongo.

Pia kuzuia uoto wa asili (magugu), kuhifadhi unyevunyevu, kuzuia mmomonyoko kwa njia ya upepo na maji na kutengeneza mazingira mazuri ya viumbe hai kama vile minyoo kuishi kwenye udongo.

Mazao yanayotambaa hasa yale yanayostahimili ukame kama vile ngwara na mukuna ndiyo yanayofaa zaidi. Mboji hutokana na kuoza kwa mimea, taka na wanyama. Kazi ya kugeuza kuwa mboji hufanywa na viumbe hai ardhini.

Mbinu ya tatu ni kilimo cha mzunguko ambapo badala ya kulima mazao yale yale kila msimu, mazao hubadilishwa msimu kwenda mwingine kwa mzunguko.

Hii ni kwa sababu mazao huhitaji viwango tofauti vya virutubisho toka kwenye udongo, kina tofauti cha mizizi, wadudu tofauti waharibifu na magonjwa tofauti.

Hatua hii hufanya matumizi mazuri ya mboji, kudhibiti wadudu waharibifu na kuzuia kuenea kwa magonjwa.

Ni vyema katika mzunguko pawepo na mimea ambayo hutengeneza naitrojeni kwenye mizizi yake (mazao aina ya mikunde) kama maharagwe, kunde, mbaazi na fiwi. Mfano wa mzunguko mmoja unaweza kuwa: mahindi – kunde – mtama.

Gharama za uzalishaji wa mazao kwa mbinu za

Kilimo-Hifadhi ni ndogo kwa sababu huondokana na kukwatua (kwa njia ya plau).

Katika kipindi cha mpito inahitajika kuvunja jasi. Hata hivyo, hufanyika kwa muda mfupi na gharama yake ni nusu ya gharama ya kulima kwa plau.

Baada ya kipindi cha mpito, gharama za kuvunja jasi huondoka. Shamba ambalo litalimwa kwa kuzingatia kanuni za Kilimo-Hifadhi, gharama za palizi nazo zitashuka kutokana na kupanda mazao funika na kuwepo kwa mabaki ya zao lililotangulia.

Mabaki haya huongeza rutuba ardhini baada ya kuoza. Pia huzuia kutiririka kwa maji ovyo na hivyo kuzuia virutubisho vya mimea kuondolewa sehemu iliyokusudiwa shambani.

Kutokana na hali hii, ni wazi kwamba uzito wa kuhudumia shamba hupungua ufanisi na uzalishaji kuongezeka.

Baadhi ya zana muhimu zinazotumika katika Kilimo-Hifadhi ni pamoja na tindo au ripa ambayo hutumika kuvunja jasi, jembe la makucha (chisel) ambalo pia hutumika kuvunja jasi, direct seeder ambayo ni kipandio maalum kwenye eneo ambalo halijalimwa na lina mabaki ya mimea (kama mabua).

Zana hizi zipo ambazo hukokotwa na wanyamakazi au trekta. Ipo pia ‘jab planter’ ambayo ni kipandio cha mkono kwa ajili ya mahindi na mbegu za mazao aina ya mikunde.

Zipo pia zana kwa ajili ya kudhibiti magugu na wadudu waharibifu.

Udhibiti wa magugu huweza kufanywa kwa kutumia zana iitwayo ‘push weeder’ ambayo husukumwa kwa mkono.

Kilimo-Hifadhi hufaa kwa maeneo yote na kwa aina zote za mazao nchini Tanzania. Ndiyo suluhisho la mkulima kuondokana na kilimo duni ambacho hakimzalishii mazao ya kutosha kwani mkulima huweza kupata mavuno mengi katika eneo dogo. Mfano: kwa upande wa kilimo cha mahindi, badala ya mavuno yaliyozoeleka ya magunia 5 hadi 10 kwa ekari, mkulima atavuna wastani wa magunia 20 hadi 25 kwa ekari.

Ni vyema sasa Kilimo-Hifadhi “kikapigiwa debe” kuwa mbinu rasmi za kilimo kwa kila mkulima nchini.

Mandishi ni msomaji wa gazeti la Pambazuko, pia ni mtaalamu wa masuala ya kilimo.

Mbunge alalama kukwama barabara

Na Mutayoba ARBOGAST, Bukoba

MBUNGE wa Missenyi, Florent Kyombo, ameiomba serikali kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Katoma-Kanyigo-Bukwali yenye urefu wa kilomita 38.8 ambayo ujenzi wake umekuwa ukisusua kwa miaka mingi.

Akizungumza bungeni wiki iliyopita, mbunge huyo alisema ujenzi wa barabara hiyo inayojengwa kwa kiwango cha lami, umekuwa ukisuasua kiasi kwamba aliwahi kumuomba Rais Samia Suluhu Hassan kusaidia kusukuma kasi ya ujenzi wake.

Tangu wakati huo hadi sasa hali imebaki ile ile ikijengwa wastani wa kilometa 0.4 kila mwaka, huku wananchi wakiendelea kulalamikia mwenendo huo wa ujenzi.

Hata hivyo, Kyombo anawapa matumaini wananchi kuwa serikali sasa imeiweka katika utaratibu wa upembuzi yakinifu na usanifu na pia imeongeza kipande cha mita 400, huku kazi za ujenzi kwa mwaka ujao wa fedha zikitengewa shilingi milioni 100.

Mbunge huyo aliishukuru serikali kwa kukamilisha baadhi ya miradi ya barabara jimboni kwake na kutoa nafuu kwa wananchi.

“Mimi nimesimama hasa kwa niaba ya wananchi wa Missenyi kutoa pongezi kwa kazi kubwa ambayo kupitia wizara hii (Ujenzi), Tanroad imefanya kazi kubwa na kazi za barabara zote ndani ya wilaya yetu ambazo ziko katika hatua ya ujenzi,” alisema Mbunge.

“Unapozungumza na watu wa kawaida huko Missenyi hasa Tarafa ya Kiziba inakopita barabara hiyo ambayo ndiyo pekee yenye kipande lami tarafani humo, hawawezi kusema wananufaika,” aliongeza.

Barabara hiyo ni muhimu kuziunganisha Tanzania na Uganda na iwapo ujenzi wake utakamilika itawaweza rahisi zaidi kusafiri kati ya Bukoba na Kampala (Uganda) kuliko barabara zinazotumika sasa na kusafiri kwa mashua kupitia ziwa Victoria.

Aliyekuwa mbunge wa Bunge la Kakuuto, wilaya ya Mbarara nchini Uganda, Kalembe Christopher, akiwa mgeni mwalikwa Desemba mwaka 2019 katika mkutano mkuu wa Umoja wa Maendeleo wa Wananchi wa kata za Kanyigo na Kashenye (KADEA), alisema kuwa ushirikiano mzuri kati ya Tanzania na Uganda, utafaidisha nchi hizo iwapo kutakuwa na uhakika wa barabara ya lami.

Alisema nchini Uganda, jitihada zinafanyika kuanzisha kivuko kwenye Mto Kagera, ingawa mpango huu unaweza kugharimu fedha nyingi.


Barabara nyingine wilayani Missenyi ambazo Kyombo ameendelea kuzipigania ni barabara ya lami kutoka Bunazi hadi kiwanda cha sukari Kagera ambayo ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 300, lakini pia katika bajeti hii imepewa shilingi bilioni 5.4 pamoja na Barabara ya Mutukula-Minziro ambayo imetengewa shilingi milioni 100.



Mbunge wa Missenyi, Florent Kyombo



Habarika kidijitali! Soma gazeti la Pambazuko na magazeti mengine maarufu kwenye Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



Habari

Mageuzi makubwa gesi asilia



Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga akikata utepe kuzindua Kituo Mama cha Gesi Asilia iliyoshindiliwa (CNG) kilichopo Ubungo na basi la mfano la Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka (UDART) ambalo litaendeshwa kwa kutumia nishati ya gesi asilia, Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu)

Na Mwandishi WETU

WIKI iliyopita Tanzania imepiga hatua kubwa katika safari ya mageuzi ya matumizi ya gesi asilia nchini.

Hatimaye serikali imetoa sehemu ya majibu kwa kilio cha muda mrefu cha wamiliki wa magari yanayotumia gesi asilia ikiwa nishati ya kuyaendesha.

Serikali ilizindua kituo kikuu cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) jijini Dar es Salaam.

Kinatajwa kuwa ni kituo cha pili kwa ukubwa cha aina hiyo katika Bara la Afrika na kikubwa zaidi katika eneo la Afrika Mashariki.

Kituo hicho kinachomilikiwa na Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania (TPDC), kilizinduliwa Mei 9, 2025, na Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga.

Uzinduzi huo umetajwa kuwa ni hatua kubwa ya kimkakati katika mnyororo wa thamani wa gesi asilia nchini na ni hatua muhimu katika ajenda ya serikali ya matumizi ya nishati safi.

Kikiwa na uwezo wa kuhudumia magari 1,200 kwa siku na kina uwezo wa kufanya kazi kwa saa 24 bila kusimama, kituo hicho kilicho-

po katika Barabara ya Sam Nujoma kinatarajiwa kuwa msaada mkubwa kwa wamiliki wa magari yanayotumia gesi asilia badala ya mafuta.

Aidha, kinatarajiwa kupunguza gharama za uendeshaji kwa watumiaji wa nishati hiyo, kupunguza uzalishaji wa hewa chafu na kuleta msukumo mpya kwa ukuaji wa viwanda nchini.

Katika hafla ya uzinduzi, pia lilizinduliwa basi la kwanza la Mwendokasi (Udart) linalotumia gesi asilia - likiwa ni dalili ya mabadiliko ya matumizi ya nishati safi katika usafiri wa umma.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Kapinga alieleza kuwa mafanikio hayo ni matokeo ya uongozi madhubuti wa Rais Samia Suluhu Hassan, katika kutatua changamoto za sekta ya nishati kwa vitendo.

Naibu waziri huyo alisifu uongozi wa TPDC kwa kusimamia mradi huo kwa ufanisi na dira.

Alieleza kuwa kituo hicho kipya chenye pampu nane, kinajibu malalamiko ya wananchi kuhusu msongamano katika vituo vilivyokuwepo kama vile Ubungo Maziwa na kinahakikisha huduma zinatolewa kwa kasi na ufanisi.

Mageuzi makubwa katika gesi asilia

Inatoka Uk. 34

Pia, Kapinga alisisitiza umuhimu wa kupeleka huduma hii ya nishati safi kwa taasisi za shule, viwanda, hoteli na hata kaya za kawaida, akilitaka TPDC kudumisha viwango vya juu vya usalama na huduma katika kituo hicho.

Aliagiza pia kuharakishwa kwa ujenzi wa vituo vingine kama hivyo katika mikoa ya Lindi, Mtwara na maeneo mengine ya kimkakati nchini.

Katika kuhamasisha matumizi ya gesi kwenye magari, Kapinga alitaja faida za kiuchumi kwa wananchi, akisema matumizi ya gesi yanaweza kupunguza gharama za uendeshaji hadi kwa asilimia 40 ikilinganishwa na petroli.

Kituo hicho kikuu cha CNG kina uwezo wa kuhifadhi na kusambaza futi za ujazo milioni 4.2 kwa siku (sawa na kilo 120,000), kikiwa na pampu nne zenye miundo ya pande mbili, pamoja na pampu tatu maalum kwa ajili ya magari yanayosambaza gesi kwa vituo vya mikoani, viwandani na majumbani.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, Francis Mwakapalila, alisema shirika hilo tayari limeanza mchakato wa kununua vituo vitano vya gesi vinavyohamishika vitakavyotoa huduma katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma - ikiwa ni ishara ya dhamira ya serikali kupanua wigo wa nishati safi kote nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya TPDC, Balozi Ombeni Sefue, aliahidi kukomesha misururu ya magari kwenye vituo vya gesi na kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa huduma hiyo kwa watumiaji wote.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Dkt. James Mataragio, alisema kituo hicho kinaonesha kiwango kipya cha uendeshaji wa miradi ya nishati safi na kukitaja kuwa ushahidi wa utayari wa Tanzania kuongoza Afrika katika matumizi ya nishati mbadala na kupunguza uchafuzi wa mazingira.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, Kilumbe Ng'enda, alisi-

fu kasi ya maendeleo ya sekta ya gesi nchini na kubainisha kuwa gesi imekuwa mbadala bora kiuchumi kwa wananchi, ikizingatiwa inabana gharama kwa kiasi kikubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Ubungo, Albert Msando, alisema serikali itahakikisha inalinda miundombinu hiyo muhimu ya kimkakati na kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma bora bila usumbufu.

Uzinduzi huu ni hatua muhimu katika mkakati wa Tanzania kuwa kitovu cha nishati safi Afrika Mashariki, ukiunganisha rasilimali za gesi asilia na mahitaji ya mijini, viwandani na katika maisha ya kila siku ya wananchi kupitia miundombinu madhubuti na inayozidi kupanuka.

Kwa muda mrefu kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wamiliki wa vyombo vya moto vinavyotumia gesi asilia kutokana na changamoto mbalimbali zinazokwamisha matumizi bora ya teknolojia hiyo ya nishati safi.

Uchache wa vituo vya kujaza gesi unasababusha foleni ndefu katika vituo vya kujaza gesi na kusababisha wamiliki wengi kutumia muda mrefu kupata huduma hiyo, hasa katika vituo kama Ubungo Maziwa.

Wakati mwingine magari hulazimika kulala usiku kucha kwenye vituo ili kupata huduma asubuhi.

Licha ya ongezeko la magari yanayotumia gesi, vituo vya kujaza CNG ni vichache mno, hasa nje ya jiji la Dar es Salaam.

Hali hii inawakatisha tamaa watumiaji wapya na kuzuia upanuzi wa teknolojia hii maeneo ya mikoani.

Baadhi ya wamiliki wanalalamika kuwa mitambo ya magari ya gesi hupata hitilafu mara kwa mara, lakini mafundi waliobobea na vipuri halali ni wachache nchini.

Wamiliki wapya wa magari ya gesi hulalamiika kutopata mafunzo sahihi juu ya uendeshaji wa magari haya na matumizi salama ya CNG.

Hali hii huongeza hatari za kiusalama na matumizi yasiyo sahihi ya mfumo wa gesi.

Aidha, wamiliki hao wamekuwa wakidai kwamba wakati mwingine bei ya kujaza gesi hubadilika bila taarifa rasmi mapema, na hakuna mfumo wa wazi wa bei kama ilivyo kwa mafuta.

Makala

Sayansi nyuma ya 'moshi wa Papa'



Na Mwadishi WETU

KAMA ilivyo desturi ya Kanisa Katoliki (RC), wiki iliyopita makardinali kutoka duniani kote walijifungia katika kanisa jijini Vatican wakifanya uchaguzi wa Papa mpya baada ya kifo cha Papa Francis.

Kwa mujibu wa utamaduni wa kanisa hilo, katika kipindi hiki cha uchaguzi wa Papa, makardinali hao wanajifungia ndani, bila ya kuwa na mawasiliano na watu walioko nje ya chumba cha mkutano.

Mawasiliano pekee kati yao na watu waliopo nje ni moshi unaotoka kwenye bomba maalum pale ambapo wamefikia uamuzi – moshi mweusi ukiashiria bado uchaguzi haujampata Papa au moshi mweupe pale ambapo kiongozi mpya wa kanisa hilo anapokuwa amepatikana kwenye uchaguzi.

Moshi huu unatokana na kura zinapochomwa baada ya kila hatua ya uchaguzi kukamilika.

Awali, moshi huu haukuwa unatolewa nje kama ilivyo hivi sasa. Hata ulipoanza kutolewa katika karne ya 18, hakuwa unatolewa kama sehemu ya ishara ya matokeo ya uchaguzi.

Lakini wakati huo watu wakaanza kutumia rangi ya moshi huo kufanya utabiri wa matokeo ya uchaguzi.

Hii ilitokana na mazoea kuwa unapotoka moshi wa aina fulani basi uchaguzi unakuwa haujakamilika na unapotokea rangi nyingine ni ishara kubwa kuwa uchaguzi umekamilika.

Lakini baada ya utamaduni wa watu kubashiri matokeo ya Papa kutokana na rangi ya moshi,

kanisa likaamua kuweka utaratibu maalum wa kuwasiliana na jamii ya watu walioko nje kwa kutumia rangi ya moshi.

Makardinali wanapokuwa kwenye uchaguzi wa Papa wamekuwa wakitumia njia mbalimbali kutengeneza moshi huu kama njia ya kuwaonyesha waumini na watu wengine walioko nje nini kinaendelea ndani.

Kwa mujibu wa Mark Lorch, Profesa wa mawasiliano ya sayansi na kemia kutoka chuo kikuu cha Hull, Uingereza, utamaduni wa makardinali kuchoma kura zao ulianza karne ya 15.

Hata hivyo, utaratibu wa kuweka bomba ambalo litautoa moshi huo nje ulianza karne ya 18.

Mwanzoni karatasi zilikuwa zinachomwa ndani na moshi kubakia humohumo.

Lakini baadaye kukawa na wasiwasi kuwa moshi huo unaweza kuwasababishia makardinali matatizo ya kiafya hasa pale karatasi za kura zinapokuwa nyingi.

Ndipo uamuzi ukafanywa kuwa liwekwe bomba ambalo litautoa moshi huo nje ya chumba hicho ili kuwalinda makardinali kiafya.

Hiyo ilisababisha watu wengine walioko nje nao kuuona moshi huo. Wakati huo jambo hilo halikulenga kuwa mawasiliano mahsusi na watu walioko nje ya chumba cha mkutano, lakini kila moshi ulipoonekana, watu walianza kutoa tafsiri na kubashiri matokeo ya uchaguzi.

Ilipofika karne ya 19, utamaduni wa kutumia moshi kama ishara ya mawasiliano ukawa umezoeleka.

Hata hivyo, hali hii ilikosa ufasaha na ikawa inasababisha mchanganyiko wakati fulani kwani ilikuwa vigumu kutambua rangi halisi ya moshi.

Baadaye, kanisa likaamua kuweka utaratibu mahsusi ili moshi huo utumike kama ishara ya mawasiliano na kutoa ujumbe kwa watu walioko nje wakisubiri matokeo ya uchaguzi.

Ndipo ukaanza kutumika moshi mweusi, ambao kitaalamu unajulikana kama 'fumata near,' kuashiria kuwa Papa hajapatikana na moshi mweupe, yaani 'fumata bianca,' kushiria kuwa Papa mpya ameshachaguliwa.

Moshi unavyotengenezwa

Siku za mwanzo, lami na vijiti vilivyoloweshwa na maji viliongezwa kwenye karatasi za kura.

Inaendelea Uk. 37

Sayansi nyuma...

Inatoka Uk. 36

Kama inavyojulikana, lami inapochomwa ikiwa na kitu kibichi, basi inakuwa vigumu sana kwa mchanganyiko huo kushika moto na jinsi mchakato wa uchomaji unavyoendelea basi hapo huzalishwa moshi mwingi mweusi.

Hii ni kemia ya kawaida. Moshi mweusi huo ni matokeo ya kutokamilika kwa tukio la uchomaji wa kitu chochote.

Katika mchakaro huu, nguvu aina ya joto hujaribu kuyeyusha maji kwenye vijiti, ambayo kwa upande mwingine yanashusha joto la moto.

Matokeo yake molekuli nyingi kubwa kwenye lami zinabakia bila kuchomwa sawasawa na kusababisha kutokea kwa jivu jeusi.

Hata hivyo, pale maji hayo yanapokuwa yamemalizika kwenye vijiti, moto huunguza mchanganyiko huo kwa ufanisi mkubwa na kutoa mvuke na hewa ya kaboni dayoksaidi, vitu ambavyo vikichanganyika na lile jivu, basi hutoa moshi mweusi.

Hata hivyo, ilikuwa ni vigumu sana kuwa na aina ya moshi ambao ungetoa ishara isiyo na shaka, kwani katika mchakato wa kuungua ungeweza pia kutoka moshi wa kijivu na kuwaacha watu na mshangao.

Lakini ilipofika miaka ya 1970, utaratibu wa kutumia vijiti ukaachwa na badala yake zikanza kutumia kemikali mahsusi ambazo zilikuwa zinatoa aina ya moshi unaokusudiwa.

Mchanganyiko wa sasa

Mwaka 2013, Vatican ilithibitisha kuwa utaratibu wa kuchoma kura unahusisha kemikali ambazo zinatoa rangi ya moshi kwa uhakika zaidi.

Kwa moshi mweusi, mchanganyiko huu unahusisha kemikali za potassium perchlorate (KClO_4), ambayo inapochomwa hutoa hewa na oksjeni. Kemikali nyingine ni anthracene, inayotokana na makaa ya mawe na lami ambayo inapochomwa hutoa moshi mzito mweusi na Sulphur ambayo huonegzwa ili kudhibiti kiwango cha joto kura zinapochomwa ndani ya mchanganyiko wa kemikali hizo.

Matokeo yake ni kama ya awali, uchomaji haukaliliki sawasawa na hivyo kuzalisha moshi mwingi mweusi na ambao ndio huonekana pale ambapo uchaguzi unakuwa haujampata Papa.

Kwa upande mwingine, moshi mweupe hutengenezwa kwa kutumia kemikali zinazoshika moto haraka.

Potassium chlorate (KClO_3) – ambayo huungua haraka – inahakikisha kuwa joto linakuwa jingi na kubwa.

Kwa upande mwingine, lactose nayo inakuwa na nishati, ikiungua haraka na kusababisha mvuke na hewa na kaboni dayoksaidi.

Uunguaji huu wa haraka kemikali hizi zenye sukari nyingi unazalisha gesi nyingi yenye kemikali aina ya pine rosin.

Kemikali hii inapokutakutana na lile joto kali, basi huzalisha moshi mzito ambao hutoa jivu lenye rangi nyeupe ambalo likiungua ndio huzalisha moshi mweupe unaoonekana nje.

Mabadiliko

Kwa miaka mingi mkutano wa kumchagua Papa umekuwa ukifanya mabadiliko ya kutoa ujumbe kwa watu wanaosubiri nje kuhusiana na matokeo ya uchaguzi.

Kwanza, utaratibu wa kuchoma kura ulianza kama jambo la kiusalama kutokana na hatari za kiafya kwa waliokuwa ndani ya chumba karatasi zinapochomwa; moshi ukaanza kuelekewa nje.

Huko nje watu wakaanza kufanya utabiri kwa kutumia moshi huo na ili kuondoa mchanganyiko kutokana na watu kutabiri vile wana-vyojisikia, Kanisa likaamua kuweka utaratibu mahsusi kwa kutumia moshi huo kama njia ya mawasiliano kati ya makardinali walioko kwenye kikao cha uchaguzi na watu walioko nje.

Hivi leo, kwa kutumia sayansi ya kemia ya kisasa, uwezekano wa kutoa aina ya moshi unaotakiwa kutoa ujumbe ni mkubwa zaidi – moshi mweusi ukitumika kueleza kuwa Papa hajapati-kana, huku moshi mweupe ukitoa ujumbe kuwa Papa mpya ameshachaguliwa.

Na unapoonekana moshi mweupe, basi watu waliopo eneo la Kanisa la Mtakarifu Petro huko Vatican, hujiandaa kumuona Papa mpya ambaye hutokea katika veranda maalumu ili kujitambulisha, kuwaomba waumini mwamuombee naye kuwabariki.

Habari katika picha



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Augustino Senga akizungumza kuhusu ushirikiano katika suala la usalama kwa wakazi wa maeneo ya mgodini, wakati alipotembelea mgodi wa dhahabu wa Anglo De Beers (T) Limited uliopo Kijiji cha Patamela mkoani Songwe kutathmini hali ya usalama na ustawi wa wachimbaji wa eneo hilo juzi. Picha na Issa Mwandagala



Waziri Mkuu Mstaafu, John Malecela, akitoa salamu za pole kwa Waziri wa Maji, Juma Aweso (wa pili kushoto) aliyefiwa na mdogo wake, Ally Aweso, mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Wetu)



Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Kata ya Iyula, Yakobo Dungu-marro, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Simbega iliyopo katika kata hiyo mkoani Songwe, akiwataka wazingatie masomo yao na kuacha tabia ya kujihusisha na uhusiano wa kimapenzi wakiwa bado ni wanafunzi, mwishoni mwa wiki. (Picha na Issa Mwandaga)



Barabara ya kuingia bandari kavu eneo la Ubungo Maziwa ikiwa imejaa maji na kushindwa kupitika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha jijijini Dar es Salaam jana. (Picha na Fidelis Felix)



Kila heri Abby Chams BET

Na Mwandishi WETU

MWANAMUZIKI wa Tanzania anayekuja kwa kasi katika anga za kimataifa, Abigail Chams (almaarufu Abby Chams), huenda akashangaza dunia ya muziki atakapoibuka mshindi katika tuzo kubwa za fani hiyo nchini Marekeni.

Juni 9, mwaka huu, ndiyo siku kutafanyika sherehe kubwa ya kutimiza miaka 25 tangu kuanza kwa Tuzo za BET, ambazo zinabeba hesima kubwa zaidi miongoni mwa tuzo za sanaa ya muziki.

Katika sherehe hizo zitakazofanyika kwenye ukumbi wa Peacock, ndani ya Jiji la Los Angeles, sambamba na utoaji wa tuzo kwa washindi, Abby Chams, atakuwa anashiriki kwa mara ya kwanza.

Abby Chams, jina lake limetajwa katika kipengele cha mwanamuziki mpya anayeibuia kimataifa (BNIA), akiwa anachuana na wanamuziki wengine kutoka Brazil, Uingereza, Nigeria, Afrika Kusini na Ufaransa.

Binti huyo anayetamba sasa na muziki wake aliomshirikisha Harmonize wa “Me Too,” ameanza kukubalika kimataifa, huku nyimbo zake katika Youtube, zikiendelea kufuatiliwa zaidi.

Wimbo wake mpya wa Me Too, kwa kipindi cha miezi miwili tayari umetazamwa na watu zaidi ya milioni 10.

Gazeti la Pambazuko pamoja na wasomaji wake, linamtakia Abby Chams kila heri, huku likihimiza aendelee kufanya kazi zake kwa weledi, staha, na kujituma zaidi.

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

**Nguo za
'Leopard
Print'
zinavyobamba**

NGUO za 'Leopard Print' au mavazi yenye rangi ya chui, zimekuwa zikibamba siku hadi siku katika suala zima la mitindo.

Nguo hizo ambazo michoro yake inashabihiana na rangi ya ngozi ya mnyama chui, zimekuwa zikivaliwa na jinsia ya kike, lakini kwa upande wa kume ni mara chache sana.

Kwa mujibu wa wabunifu wa nguo, rangi ya chui zina maana yake na hunasibishwa na tabia zinazohusu watu wanaovaa nguo hizo.

Inaelezwa kuwa kuvaa nguo hizo ni ishara ya utajiri, huvaliwa na kutumiwa na wafalme na malkia. Chui mara nyingi wamekuwa ishara ya ujasiri na ukali.


Watu maarufu duniani na hata wanamuziki wamekuwa wakivaa vazi hilo, akiwemo Beyonce ambapo katika albamu yake ya 'black is king' alivaa vazi hilo la 'Leopard Print' huku akieleza kuwa ilichukua saa 1000 kuitengeneza.

Namna ya kupangilia

*Vaa nguo hizi kwa kuchanganya na nguo zenye rangi nyeusi, nyeupe, nyekundu na kahawia.

*Kwa mtoko wa usiku; vaa rangi ya chui yenye kitambaa cha satini au velveti.

*Kwa ofisini; vaa rangi ya chui ikiwa na kitambaa cha pamba ili kuzua joto. *Kipindi cha baridi; vaa ikiwa na mtindo wa 'leather' kwa kuwa inasaidia kukinga baridi.

**Fanya hivi
kutibu ngozi
iliyoharibika**

WANAWAKE wen-gi ambao wanatumia vipodozi vikali, mara nyingi wanaharibika ngozi.


Ili kutibu tatizo hilo fanya yafuatayo;

*Chukua parachichi lililoiva vizuri, kicha lisage.

*Pakaa mchangan-yiko huo sehemu ya ngozi iliyoharibika, iache kwa dakika tano halafu safisha vizuri uso wako.

*Fanya hivi mara mbili kwa wiki kwa matokeo zaidi.

**Kwa maoni na ush-
auri: piga simu
0656531217**



Na Anti
MSHAURI



Uhusiano



Usidharau urafiki, utakufikisha mbali

BILA shaka u-mzima msomaji wangu wa safu hii ya uhusiano. Karibu tuhabarishane masuala mbalimbali kuhusu maisha.

Leo nitazungumzia mambo ya kuzingatia kwenye urafiki.

Kwenye maisha kila mtu anamuhitaji mwenzake kwa namna moja au nyingine. Kuna wakati unamuhitaji rafiki wa kupeana mawazo, ushauri na mambo mengine muhimu.

Marafiki ndio wanaoweza kukupa msaada pale unapouhitaji, faraja, unapopitia kwenye kipindi kigumu na kadhalika.

Ili urafiki wowote ukue unategemea wahusika kuwa na usawa katika kufanyiana mambo kwa usawa iwapo mmoja wenu anapata tatizo au jambo la furaha.

Ikiwa marafiki mtashikamana kwa kushirikiana katika mambo mbalimbali, itawasaidia kufika mbali.

Kuna mfano wa marafiki wengi ambao kushikamana kwao kumewafanya kuwa na uhusiano mzuri kiasi cha familia zao kuwa pamoja kwenye matatizo na furaha.

Kuna watu huanza urafiki tangu wakiwa shule na kuimarika kwa urafiki wao hujikuta wakisonga mbele pamoja hata katika maisha yao ya kujitegemea; hilo ni jambo jema.

Urafiki wa kweli ni tunu inayopaswa kulindwa na kuheshimiwa.

Tukutane wiki ijayo...

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.

Burudani

Wasanii na mikataba ya kinyonyaji



Na Mwandishi WETU

'RECORD LABEL' imekuwa kama fasheni kwa wasanii wengi wa Bongo Fleva, kila msanii aliyefanikiwa, anaanzisha rekodi lebo naye anasaini na kusimamia wasanii.

Kuwa na rekodi lebo siyo jambo baya, ila wasanii wengi nadhani hawaelewi maana yake au hawana uwezo wa kuwa na hizo rekodi lebo kama za wasanii wa nchi zingine ikiwamo, Nigeria.

Ukiongelea rekodi lebo za Nigeria, lazima utaitaja Marvin Record inayowasimamia wakina Rema, Ayra Starr, pia kuna YBNL inayomsimamia Fire Boy, Asake, na wengine wengi.

Diamond Platnumz ni miongoni mwa wasanii wa mwanzo kuanzisha rekodi lebo na wasanii wengi kuiga kama Alikiba, Harmonize, Nandy, lakini wameshindwa kuendeleza vipaji

wanavyovisaini katika lebo zao matokeo yake kuwaacha wasanii hao njia panda hatuoni muendelezo mzuri kama kwa wenzetu.

Sakata la Ibrah ndio limenifanya niandike na kuhoji hivi wasanii wanaelewa mikataba wanayoingia kweli?

Basata na Cosota wanapaswa kuwasaidia wasanii wetu kuwapa elimu ya mikataba pamoja na thamani yake.

Wasanii wakitaka kutoka kwenye lebo wanatajiwa dau kubwa la fedha ili kuchomokoa kwenye mikataba.

Mfano mzuri ni Harmonize wakati anatoka lebo ya WCB, aliambiwa alipe milioni 600 na sasa yeye pia anamwambia msanii wake alipe shilingi bilioni 1.

Swali la kujiuliza ni hili, je, Ibrah ana thamani hiyo au anamkomoa tu huyu kijana asiendelee na harakati zake za muziki?

Rihanna kupata mtoto wa tatu

Na Mwandishi WETU

UPO mstari katika Biblia unaosema; "nendeni mkaijaze dunia." Huu ume-wakaa mno wasanii; Rihanna na A\$AP Rocky, ambao sasa wameamua kuijaza dunia tu.

Wawili hawa watarajia kupata mtoto wao wa tatu. Riri ameonesha rasmi ujauzito wake kupitia onesho la MetGala usiku moja wa wiki iliyopita.

Pamoja na A\$AP Rocky, wawili hao wana watoto wawili tayari; RZA ambaye alizaliwa Mei, 2022 na Riot aliyezaliwa Ago-sti, 2023.



Hersi, Yanga...

Inatoka Uk. 44

Ukisoma kanuni ya 13 ya FIFA inasema kuwa mkataba wa mchezaji na timu utatamatika tu pale unapoisha au kwa makubaliano kati ya pande zote, lakini tulichoona kati ya Fei Toto na Yanga, ni uhuni ambao kwa bahati mbaya baadaye ukalinishwa na siasa.

Lakini haikuishia hapo, tathmini inaonyesha kuwa Yanga walihamasisha uhuni kama huo kwa Prince Dube, mchezaji halali wa Azam ili kulipa kisasi katika mtindo kama huo.

Hata kama Yanga walilipa kisasi, (na tunasema kisasi ni halali), lakini lazima tukubaliane hapa kuwa Dube kugomea kuutumikia mkataba wake na kisha kulazimisha kuhamia Yanga ni uhuni na hauhitajiki kwenye soka la kisasa.

Kwa mfano, mimi naamini kama Kocha Nabi angekuwa na Feisal kwenye timu yake kwenye fainali ya Kombe la Shirikisho, huenda Yanga wangekuwa mabingwa, kwa kuwa sote tunajua Fei Toto ana uwezo wa kuchangia matokeo chanya kwa nafasi yake.

Pili, nizungumzie kampuni ya GSM ambayo ni mdhamini mkuu wa Timu ya Yanga, na kudhamini timu zingine kadhaa katika ligi hiyohiyo.

Katika mahojiano yake na Wasifi TV Augusti 21, 2024, Hersi aliulizwa hili swali la mgongano wa masilahi kati ya Yanga na GSM na akalijibu vizuri, kwamba hakuna ushindani wowote kati ya Yanga na GSM na hivyo tunamchukulia GSM kama mfadhili anayeiwzesha Yanga ili GSM atangaze biashara zake.

Lakini sidhani kama jibu hili linafaa pia kuise-mea Singida Black Stars, Namungo, Mashujaa, Coastal Union, ambazo GSM anazidhamini na tunaambiwa Hersi bado ni mkurugenzi wa uwekezaji wa Kampuni ya GSM na wakati huo-huo ndiye Rais wa Yanga.

Je, Yanga hazishindani na hizo timu ambazo Hersi na kampuni ya GSM inazidhamini? Katika hali ya kawaida hakuna utetezi, kuna mgongano wa masilahi wa wazi na unaathiri kile tunachokii-ta 'uwanja sawa wa mashindani' kwenye soka.

Ifahamike kuwa timu hizi kupata udhamini ni jambo jema sana, na kwa hakika kila mdau wa

soka angependa zipate wadhamini zaidi ili zikue, lakini kama mdhamini ni GSM, basi Hersi iache GSM abaki na urais wa Yanga tu, ili kule GSM wafanye uamuzi watu wengine ili kuondoa huo mgongano wa masilahi.

Kuna wazee wa Simba wamelalamika sana kuhusu jambo hili, na wanaenda mbali kutuhumu kuwa Yanga imekuwa ikipata matokeo chanya zaidi kwa hizo timu zinazodhaminiwa na GSM kwa kuwa hakuna ushindani wa kweli.

Katika mazingira kama haya, hoja zao zina mashiko na unaweza kukosa majibu sahihi zaidi ya kusema ni uhuni tu katika soka ndo unaendelezwa. Tatu, nizungumzie sakata la mechi namba 184 kati ya Yanga na Simba. Sote tunajua kuwa maandalizi yalikuwa yanaenda sawa mpaka pale Simba walipozuiliwa kuingia uwanjani Machi 7 ili wapate fursa ya kujipanga kimbinu kabla ya siku ya mtanange Machi 8, 2025.

Simba walikuwa na haki kwa mujibu wa Kanuni ya 17(45) za ligi Kuu Bara. Haya sababu inayotolewa ni kuwa Simba haikutoa taarifa kuwa wataenda kufanya mazoezi siku husika kwa mujibu wa 'taratibu' za Bodi ya Ligi; au kuwa Simba walienda kutaka kufanya uloji (kitu ambacho tunakiona na kusikia sana katika soka la Afrika), hazihalalishi Yanga ipeleke mabaunsa kuzuia Simba wasiingie uwanjani.

Kufanya hivyo ni uhuni, ambao mtu yeyote makini hawezi kuufumbia macho.

Bila shaka Simba walifanya kosa, kutoa tamko la kususia mechi, lakini kanuni ya 31(1) bado inatoa kinga kwa timu itakayoshindwa kwenda uwanjani kama tu itatoa sababu ya msingi.

Na sababu ya Simba inagusa 'usalama,' kitu ambacho kinapewa kipaumbele kikubwa katika soka duniani. Kwa hiyo, Bodi ya Ligi ilibidi ijitathmini, aidha kuingia kwenye mgogoro na Simba kwa kulikataa tamko lao, na kuwaadhibu kama wasingepoleka timu uwanjani au wachukue madaraka yao kama wasimamizi wa soka kwa mujibu wa kanuni ya 12 (1)- (10) waahirishe mchezo ili kuweka mazingira bora ya marudio ya mechi, ambapo hilo la pili likawa rahisi kwao.

Kinachoshangaza ni kuwa pamoja na kuwa Bodi ya Ligi ilitoa tangazo la kuahirisha mechi, ikimaanisha maofisa wa mechi wote hawakuja uwanjani, bado uongozi wa Yanga ulipeleke timu uwanjani.



Hersi, Yanga wajitafakari zaidi



Na Dkt. Richard MBUNDA

NIKIWA mpenzi wa soka, lazima nikiri kuwa 'namzimia' sana Mhandisi Hersi Said, Rais wa Yanga.

Ninavutiwa zaidi na maono yake ikiwemo kuhakikisha Yanga inakuwa na uwanja wake unaoaweza kubeba angalau watazamaji 20,000 ndani ya miaka minne ya uongozi wake.

Hakika, hizi ni ndoto kubwa na unatamani mtu kama huyu apate msukumo wa kuzitekeleza na siyo kuanza kugombania Uwanja wa KMC ambao kimsingi ni wa hadhi ya chini sana kwa

timu kongwe kama Yanga na Simba.

Ama kwa hakika, watu 'wanaohusudu' uongozi wa Hersi ni wengi, na wengine ni mashabiki kindakindaki wa Simba.

Mbali na ujenzi wa uwanja huo, uongozi wa Hersi umejitana baisha uwanjani, kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, Yanga imekuwa ikicheza vizuri ikichukua makombe yote muhimu nchini na ilifanikiwa kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho mwaka 2023.

Kila mtu anajua kuwa kamwe huwezi kuyatenganisha mafanikio haya ya Yanga na Hersi.

Mafanikio yamejenga tabia ya kujitanga za, na ndiyo maana Hersi alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kwanza wa Chama cha Vilabu Afrika - African Club Association (ACA) mwaka 2023, akiendelea kukuza jina lake, jina la Yanga na kupeperusha bendera ya Tanzania katika tasnia ya soka Afrika.

Hata hivyo, Waswahili wanasema viongozi bora hupimwa wakati wa misukosuko. Na kwa hakika, misukosuko wanayopitia Yanga hivi sasa ni kipimo cha moto juu ya Uongozi wa Hersi na wasaidizi wake.

Kwa nafasi yake, akiwa Mwenyekiti wa ACA, ana wajibu wa kuhakikisha mpira wa Afrika unasonga mbele.

Moja ya malengo ya ACA ni kuboresha mpira wa Afrika katika nyanja zote kuwa wa viwango vya kidunia, lakini nimkumbushe tu Hersi kuwa mwishoni mwa mwaka 2022, mchezaji wa Yanga Feisal Salum, almaarufu Fei Toto, aligoma kuutumikia mkataba wake Yanga.

Inaendelea Uk. 43